epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0581870
Jumapili Novemba 24, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
0677 020 710
LIKE & FOLLOW US

UKURASA WA 2

**Waziri** ashangaa waombaji kiduchu ajira kwa mikoa ya pembezoni



UKURASA WA 3

**Lissu** awaangukia mawakili msaada kwa wagombea walioenguliwa

UKURASA WA 11

MAISHA YALIVYO

**Uhusiano** ndoto usiku na matatizo ya watu wengi




UKURASA 22

**Messi kubakia Inter Miami mpaka 2026**

# Mbowe atema nyongo

• **Ni** baada ya kuachiwa kwa masharti, Sugu asema ni njama... *Ukurasa 2*




Kiongozi mstaafu wa ACT Wazalendo, Zitto Kabwe (kushoto), akimnadi mgombea wa nafasi ya uenyekiti wa kijiji cha Nyarugusu, kata ya Kizazi, jimbo la Muhambwe, mkoani Kigoma kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Mersiana Damas, baada ya chama hicho, kutosimamisha mgombea kijijini hapo, wakati wa mkutano wake wa kuwanadi wagombea wa nafasi mbalimbali za uchaguzi wa serikali za mitaa kupitia ACT Wazalendo, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

RIPOTI MAALUM

## Mhitimu shahada ya uzamili aliyegeukia biashara chakula

UKURASA 4

## Kampeni uchaguzi S/ Mitaa zapamba moto kila kona nchini

UKURASA 3



Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) , Itikadi, Uenezi, Siasa na Mafunzo, CPA Amoss Makalla, akizungumza na wananchi wa Jimbo la Kibamba, jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni mwendelezo wa mikutano yake ya kampeni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji, unaotarajiwa kufanyika Novemba 27 mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

MICHEZO **FADLU: TUTAIMALIZA BRAVOS** UK.24 **MAONI,** UK.6

# Waziri ashangaa waombaji kiduchu ajira pembezoni

**Na Lusungu Helela,** MPANDA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu, ameshangazwa na idadi ndogo ya waombaji wa nafasi za kazi kada ya afya waliokuwa wameomba katika mikoa ya Kigoma, Katavi, Lindi na Mtwara.

Wakati waombaji katika mikoa hiyo ikiwa ndogo, mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Dodoma ina idadi kubwa ya waombaji kulinganisha na uhitaji.

Hatua hiyo imetokana na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kuweka utaratibu wa kuomba ajira katika mkoa husika kulingana na uhitaji.

Juni, mwaka huu, sekretarieti hiyo ilitangaza nafasi za kazi 9,483 za kada ya afya na kila mwombaji alitakiwa kuomba ajira katika mkoa ambao atafanya kazi endapo atafanikiwa kupita kwenye usaili.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri, licha ya tatizo kubwa la ajira linalowakumba vijana wengi, bado waombaji wanataka kuanza kufanya kazi katika majiji makubwa jambo ambalo ni gumu

Sangu alisema hayo juzi alipozungumza na watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, mkoani Katavi, ikiwa ni mwendelezo wa kliniki ya kimkakati ya kusikiliza na kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali zinazowakabili watumishi hao.

Alisema mkoa wa Kigoma, kwa mfano, mahitaji halisi ya waliotakiwa kuajiriwa katika kada ya afya yalikuwa watumishi 400 lakini waombaji wa nafasi hizo walikuwa hawazidi 200 huku mikoa ya Lindi, Mtwara na Katavi nako idadi ikiwa ndogo kulinganisha na uhitaji.

Kutokana na hali hiyo, Sangu alitoa wito kwa wazazi kuwashawishi watoto kuomba ajira pindi zinapotangazwa katika mikoa hiyo kwa kuwa uwezekano wa kupata ni mkubwa kulinganisha na mikoa kama Arusha na Dodoma ambako ushindani ni mkubwa.

Aidha, Sangu aliwaonya wale watakaoomba kazi katika mikoa hiyo halafu wakapangiwa wanaanza kuomba uhamisho. Alisema serikali haitawavumilia endapo wataanza kufanya hivyo kabla ya kufanya kazi kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu.

Naibu Waziri alisisitiza kuwa mikoa hiyo haina tofauti na Mwanza, Dar es Salaam, Dodoma na Arusha kwa kuwa ina fursa za kiuchumi na miundombinu iliyoboreshwa. Aliwataka uhitaji wa ajira kuchangamkia zinapotangazwa kwenye mikoa hiyo.

Awali, Katibu Tawala wa Mkoa wa Katavi, Abert Msovela, alisema licha ya uwapo wa fursa za kiuchumi katika mkoa huo, bado idadi ya watumishi wa umma wanaotuma maombi ya kutaka kuhamia ni kubwa.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations @guardian.co.tz***

# Mbowe atema nyongo baada ya kuachiwa

**Na Moses Ng'wat,** MBOZI

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, pamoja na wafuasi 11 waliokuwa wanashikiliwa na polisi, wameachiwa kwa dhamana, huku akisema haoni sababu mahsusi za kushikiliwa kwao.

Juzi mchana, Mbowe na wafuasi 12 walikamatwa na Jeshi la Polisi mkoani Songwe kwa madai ya kufanya mkutano wa kampeni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika eneo ambalo hawakupangiwa. Kwa kufanya hivyo, ilielezwa kuwa ni kinyume cha ratiba za wasimamizi wa uchaguzi.

Aidha, Mbowe alithibitisha kwamba Mdude Nyagali, mfuasi mwandamizi na mwanaharakati mwenye ushawishi mkubwa katika chama hicho, anaendelea kushikiliwa na jeshi hilo.

Akizungumza baada ya kuachiwa, Mbowe alisema licha ya kushikiliwa kwa muda, polisi hawajawapa sababu mahsusi za kuwakamata na badala yake wamekuwa wakisingizia mambo aliyoita yasiyo na mashiko.

"Lakini hatimaye usiku huu baada ya kudai kwa nguvu sana wametuachia na wanasema kosa letu ni kuharibu ratiba ya mikutano ya kampeni. Sasa tumeharibu vipi? Sisi hatujui.

"Tumegoma kutoa maelezo yoyote na tuliwaambia kwamba tutakuwa tayari kutoa maelezo hayo kama watatuhakikishia kuwa watatufikisha mahakamani," alisema.

Mbowe amelishutumu Jeshi la Polisi mkoani Songwe kwamba limemkamata kama mkakati wa makusudi wa kuvuruga mikutano yake ya kampeni iliyopangwa katika majimbo ya Mbozi, Vwawa na Tunduma.

**KAULI YA SUGU**

Akizungumza jana katika mkutano wa hadhara Kyela mkoani Mbeya, Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Nyasa, Joseph Mbilinyi, maarufu kama Sugu, alisema kukamatwa kwao kunatokana na hofu ya Chama Cha Mapinduzi CCM kuondolewa madarakani.

Sugu alisema CCM haikubaliki na Watanzania ndiyo maana inaogopa kuondolewa madarakani, hivyo imeamua kutumia vyombo vya dola kuwakamata viongozi wa upinzani, hususan wa CHADEMA.

"Hivi sasa kazi tuliyo nayo ni moja tu ya kuiondoa CCM madarakani kwani imechoka na haikubaliki ndiyo maana inatumia mabavu kutisha wananchi na kutumia vyombo vya dola kuwakamata viongozi wa CHADEMA.

"Ukweli ni kama walivyofanya jana (juzi) kule Songwe walipotukamata mimi na Mwenyekiti Mbowe pamoja na viongozi wengine na 'staff' (maofisa) wa Mwenyekiti. Hawana hoja ya maana, hivyo wameamua kutumia mabavu kuendelea kubaki madarakani," alisema Sugu .

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Augustine Senga, alisema jana wanaendelea kumshikilia Nyagali kwa sababu ya kuwa na mashtaka mengine, lakini akitekeleza masharti ya dhamana watamwachia.

Alisema viongozi na wafuasi wa chama hicho walioachiwa watatakiwa kuripoti tena polisi Novemba 28, mwaka huu, kama masharti ya dhamana yanavyoelekeza.

Viongozi wengine walioachiwa ni Mwenyekiti wa chama hicho, Kanda ya Nyasa, Joseph Mbilinyi, maarufu kama Sugu, Mbunge mstaafu wa Mbozi, Paschal Haonga, na Mwenyekiti wa Chama cha ACT Wazalendo mkoani Songwe, Elia Zambi.

Wafuasi wa chama hicho waliokamatwa juzi ni Adamu Kasekwa (35), Halfan Mbire (37) na Mohammed Ling'wanya (walinzi).

Wengine ni waandishi wa habari wawili, Apolinary Margwe na Keneth Ndabila pamoja na Paul Joseph (ofisa wa chama) na Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Mbozi, Michael Msongole.

Juzi, Jeshi la Polisi Mkoa wa Songwe, liliwakamata viongozi na wafuasi 12 akiwamo Mbowe kwa madai ya kufanya mkutano wa kampeni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika eneo ambalo hawakupangiwa jambo ambalo ni kinyume cha sheria na ratiba za wasimamizi wa uchaguzi.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations @guardian.co.tz***



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akimwapisha Mattar Zahor Masoud kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ikulu jijini Zanzibar jana. Katikati ni Katibu Mkuu Kiongozi Zanzibar, Mhandisi Zena Ahmed Said. **PICHA: IKULU**

# Saba wafariki ajali ya bajaji na lori

**Na Moses Ng'wat,** TUNDUMA

WATU saba wamefariki dunia baada ya bajaji waliyokuwa wakisafiria kugongana uso kwa uso na lori eneo la Mpemba, Tunduma wilayani Momba, mkoani hapa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Augustine Senga, alisema jana ajali hiyo ilitokea juzi saa 3:15 usiku, wakati dereva wa bajaji yenye namba za usajili MC 783 DUF akijaribu kuyapita magari mengine yaliyokuwa mbele yake.

Alisema dereva wa bajaji hiyo, Emmanuel Hakimu, ambaye ni mmoja wa watu saba waliofariki dunia katika ajali hiyo, alikuwa akitokea eneo la Mpemba kwenda mjini Tunduma.

Alisema bajaji hiyo iligongana na lori aina ya Scania lenye namba T 958 BCS na kwamba watu watano walifariki dunia papo hapo na wengine wawili, akiwamo mtoto wa miaka miwili, Isack Mambwe, walifariki dunia wakati wakipatiwa matibabu.

Kamanda Senga aliwataja wengine waliofariki dunia kuwa ni Rehema Christopher (25) mkazi wa Msongwa, Festo Mambwe (57) mkazi wa Mbeya, Rosemary Njema (44) mkazi wa Ipito mjini Tunduma na Milembe Siyantemi (36) mkazi wa Kapele, wilayani Momba.

Kamanda Senga alisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi ili kubaini chanzo cha ajali hiyo, huku wakiendelea kumtafuta dereva wa lori ambaye alitoweka baada ya tukio hilo.

"Miili ya marehemu imehifadhiwa katika Kituo cha Afya Tunduma. Chanzo cha ajali hii bado tunakichunguza ikiwa ni pamoja na kumsaka dereva wa Scania," alisema. Kamanda Senga aliwataka madereva na wamiliki wa vyombo vya moto kujenga tabia ya kukagua vyombo vyao kabla ya kuanza safari na kuzingatia sheria za usalama barabarani wakati wote ili kuzuia ajali zinazoepukika.

# Lissu awaangukia mawakili msaada walioenguliwa

**Na Waandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amewaomba mawakili nchini kusimama na kufungua mashauri yenye maslahi kwa umma kuwatetea wagombea wote walioenguliwa katika kinyang'anyiro cha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa bila kufuata vigezo vya kikanuni ili haki ichukue mkondo wake.

Lissu alitoa ombi hilo juzi jijini Mwanza katika mwendelezo wa ziara yake ya kuwanadi wagombea wa chama hicho katika nafasi mbalimbali za uongozi kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa.

Alisema kuwapatia msaada wa kisheria wote ambao wanahisi hawakutendewa haki wakati wa mchakato mzima wa kupata wagombea katika uchaguzi huo kinyume cha sheria na kanuni, kutasaidia hatua muhimu kuchukuliwa na kuwafanya wananchi kupata machaguo yao sahihi.

Alitaja wakati huu kuwa si wa mawakili kuwa na upendeleo kwa chama chochote kile cha kisiasa bali kuonyesha ukakamavu na utumishi wao kwa jamii katika kusaidia upatikanaji wa haki kwa wale wote wanaodhani waliondolewa bila kufuata vigezo vya kikanuni.

Lissu alisema chama hicho katika wilaya ya Nyamagana, kimesimamisha wagombea nafasi ya Mwenyekiti 165, walioenguliwa 11 huku wajumbe wakiwa 924 na walioenguliwa ni 24. Kwa wilaya ya Ilemela, alisema walisimamisha wagombea 131 nafasi ya mwenyekiti na kati yao, wanane walienguliwa huku nafasi ya wajumbe zikiwa na wagombea 694 na 10 wakienguliwa.

"Ninaifahamu vizuri wilaya hii ya Tarime kwa zaidi ya mika 20. Nimeoa huku, nimefanya kampeni na kina marehemu Chacha Wangwe. Migogoro ya Nyamongo ninaifahamu sana. Tutahakikisha tunatetea haki zenu ili kuipata Tarime Mpya," alisema Lissu.

Aidha aliwataka wanachama wa CHADEMA kujitokeza kwa wingi katika kipindi cha kampeni na wakati wa uchaguzi ili kuondoa malalamiko ya kupata viongozi wasiofaa baada ya kukamilika kwa uchaguzi.

**BITEKO APIGA KIJEMBE**

Wilayani Mbogwe mkoani Geita, Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Dk. Doto Biteko amevikejeli vyama vya upinzani kuwa hakuna chenye nia ya kufanya kazi na kuwaletea maendeleo kama ilivyo CCM bali wanahitaji vyeo kwa ajili ya kujitambulishia kwenye misiba au kwenye harusi wakialikwa.

"Hoja zetu Chama Cha Mapinduzi ni maendeleo yenu na kutaka kuondoa umasikini miongoni mwa watu na hili ndilo jambo ambalo tunaendelea kulisukuma. Nimekuja kuwaambIa hapa kuwa hakuna mtu atakayeshinda bila kupigiwa kura, hivyo kama mlivyoenda kujiandikisha, vivyo hivyo jitokezeni pia kupiga kura," alisema Dk. Biteko ambaye pia ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati.

Pia alisema alisema chama hicho hakihitaji wala hakitajihusisha na ushindi wa kubebwa kwani wanahitaji ushindi halali kutoka kwenye sanduku la kura.

**AHADI HUDUMA BORA**

Wilayani Kahama, Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya, Mussa Bukango, akinadi wagombea wa chama hicho alisema endapo wangombea wake watapata ridhaa ya kuongoza serikali za mitaa, vijiji na vitongoji, watahakikisha wanatoa huduma bora kwa wananchi pasina kupokea fedha ya aina yoyote kama ilivyozoeleka.

Alisema, endapo atabainika kiongozi kutoka chama hicho akipokea fedha kutoka kwa wananchi wanaofika ofisini kupata huduma watamwajibisha kwa kumnyang'anya kadi ya uanachama na kukosa sifa, kwani viongozi wasiokuwa waadilifu wamekuwa wakitumia mwanya wa kuomba rushwa kwa wananchi ndipo wawahudumie hilo wao wanalipiga marufuku.

Kampeni za uchaguzi wa serikali za mitaa zinaendelea katika maeneo mbalimbali nchini ambako jana jioni wilayani Kahama mkoani Shinyanga Naibu Katibu Mkuu Zanzibar kutoka Chadema, Salum Mwalimu alifanya mkutano uliowakutanisha wananchi na wanachama wa chama hicho wilayani humo akiwanadi wagombea wa chama hicho.

**Imeandaliwa na Vitus Audax, Remmy Moka (MWANZA), Shaban Njia (KAHAMA), Samson Chacha (TARIME)**

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations @guardian.co.tz***

# Kampeni uchaguzi S/Mitaa zashika kasi

**Na Waandishi Wetu**



Wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wakizunguka na gari katika mitaa ya Malamba Mawili Mbezi, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, kufanya kampeni, kwa ajili ya uchaguzi wa viongozi wa serikali ya mtaa wa King'azi B. **PICHA: SABATO KASIKA**

KAMPENI za uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopangwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu, zimepamba moto huku vyama vinayoshiriki vikinadi sera na wagombea wao ili kushawishi wananchi kuwachagua.

Wakati kampeni hizo zikiendelea, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimesema hakitacheka na mtu katika kushika dola huku Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kikidai kuwa chama tawala kinategemea vyombo vya dola kuwakamata na kutaja sababu tano za kukiondoa madarakani CCM.

Aidha, Chama cha ACT Wazalendo jana kilimnadi mgombea wa CHADEMA na kueleza kuwa adui wa vyama vya upinzani ni chama tawala.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, CPA Amos Makalla, akiendelea na ziara yake ya kampeni mkoani Dar es Salaam, akiwa jimbo la Kibamba jana, alisema wamejipanga kuhakikisha wanashinda kwa kishindo.

"Katika uchaguzi huu wa Serikali za Mitaa tutashinda na tunataka ushindi wa kishindo na kwa namna ambavyo CCM tumejipanga ni sawa na kusema yanayoendelea ni sawa na kusema yajayo yanafurahisha," alisema.

Makalla alisema CCM inauchukulia uchaguzi huo kwa umuhimu mkubwa kwani inatambua kazi ya chama cha siasa ni kushika dola na Chama hicho kinaanza na kushinda uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

"Kazi ya chama cha siasa kilichosajiliwa ni kuhakikisha kinashika dola maana kazi ya kuhubiri kwenda mbinguni hiyo inafanywa na viongozi wa dini.

"Kwa kutambua umuhimu wa kushika dola ndio maana katika uchaguzi huu CCM imeweka wagombea wake kwa asilimia 100, kwani hakuna mtaa, kijiji wala kitongoji ambacho tumeacha, kote tumesimamisha wagombea kwa nafasi zote," alisema.

Alisema vyama vingine havina utayari ndio maana wameshindwa kusimamisha wagombea katika nafasi zote na mpaka sasa kuna mitaa ambayo tayari wagombea wake hawana washindani.

Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, katika mkutano wa hadhara uliofanyika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Ipinda wilayani Kyela, Mbeya aliwakumbusha wanachama wake kuhusu misingi minne muhimu inayosaidia chama hicho kuendelea kusimama imara na kushinda.

Aliwataka viongozi wake kusimamia haki kwa wote bila kujali itikadi za vyama vya kisiasa, aliongeza kuwa kila mwananchi anapaswa kuwa na uhuru wa kufanya shughuli zake kwa furaha na amani.

Alisema demokrasia inahitaji viongozi wachaguliwe kwa njia ya kupigiwa kura na wanapaswa kuwa na hofu ya Mungu ili kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia maslahi ya wananchi.

"CHADEMA bado ni chama imara licha ya fitina tunazokutana nazo. Tunapambana hatukati tamaa. Ninatoa pongezi kwa wananchi wa Ipinda na wagombea wao kwa kushiriki kikamilifu katika mchakato huu kati ya vitongoji 30 vya mji huu," alisema.

Alisema wamefanikiwa kusimamisha wagombea 27 akisema ni hatua kubwa kwao na kwenye vijiji na mitaa bado wamefanya vizuri.

Akirejelea mafanikio ya kihistoria ya uchaguzi wa 2015 ambao walipata zaidi ya madiwani 1,200 na kushinda nafasi nyingi za ubunge, alithibitisha nguvu ya chama hicho licha ya kukosa dola.

Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Nyasa, Joseph Mbilinyi (Sugu), alisema ajenda kuu ya chama chao ni kukiondoa CCM madarakani akieleza kwamba kimeshindwa kutimiza matarajio ya wananchi.

Alisema hali ya maisha imekuwa ngumu na serikali imeshindwa kutoa huduma bora za matibabu na kuhakikisha huduma za kijamii zinapatikana kwa bei nafuu," alisema.

Sugu alitaja sababu tano za kuking'oa CCM madarakani kuwa ni viongozi wake kutochaguliwa kihalali, kushindwa kufanya vikao vya uwazi vya mapato na matumizi na kudai kimeuza huduma za mihuri ya vijiji.

Kadhalika alisema kutumia michango ya misiba kwa manufaa yao binafsi na kutumia fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwa upendeleo, huku wakikandamiza vyama vya upinzani kwa kutopewa mgao wa fedha hizo.

**ACT WAZALENDO**

Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Dorothy Semu, akihutubia wakazi wa kijiji cha Milola A, Kata ya Milola, jimbo la Mchinga mkoani Lindi, aliwataka wananchi kuchagua viongozi watakaoshirikiana nao kujiletea maendeleo akiwamo Abdallah Shedafa.

Kiongozi mstaafu wa chama hicho, Zitto Kabwe, akiwa katika kijiji cha Bunyambo, jimbo la Muhambwe, alisema wananchi wanakabiliwa na tatizo kubwa la maji ambalo linaweza kutatuliwa kwa viongozi wa vijiji kukaa na mamlaka za maji, kuzitatua. Alisema CCM inapuuza changamoto ya maji inayowakabili wananchi.

Naibu Waziri Kivuli wa Viwanda na Biashara wa chama hicho, Julius Masabo, alimnadi mgombea wa uenyekiti wa CHADEMA, Marisiana Damasi, katika Kijiji cha Nyarugusu, Kata ya Kizazi, jimbo la Muhambwe na kusema adui wa upinzani ni CCM.

Alisema ACT Wazalendo, ilimnadi mgombea huyo kwa kuwa haijasimamisha mgombea kwenye nafasi ya uenyekiti kijijini hapo.

"Tushirikiane kuhakikisha tunaifuta CCM kwenye Kijiji chenu. Mpeni kura mama Merisiana na wajumbe wa ACT Wazalendo tuliowasimamisha," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa ACT Wazalendo (Bara), Isihaka Mchinjita, akiwa katika kijiji cha Kiwalala, jimbo la Mtama, alisema CCM imevigeuza vijiji kuwa makazi ya maskini kwa kusimamia mapato na matumizi ya vijiji kwa usiri.

Aliwataka wananchi kuchagua wagombea wa chama hicho, ili wasimamie mapato kwa uwazi na kwa maendeleo ya wanakijiji wote.

**•Imeandikwa na Romana Mallya, Restuta James na Grace Mwakalinga.**

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations @guardian.co.tz***

# Mhitimu shahada ya uzamili aliyegeukia biashara kupika

## -Chanzo ni ugumu kupata ajira, atoa ushauri kuntu

**Na Restuta James**

UHABA wa ajira nchini bado ni tatizo. Baadhi ya wanasiasa walishasema ni bomu linaloweza kulipuka wakati wowote. Ni jambo ambalo si tu limeongeza umaskini bali hata baadhi ya watu kuamua kujitoa uhai kwa sababu ya msongo wa mawazo uliosababishwa na ukosefu wa ajira.

Baadhi ya wahitimu wako mitaani wanarandaranda kusaka ajira. Hata baadhi ya walioajiriwa hawafanyi kazi kulingana na fani walizozisomea.

Ester Mgidula (26), mhitimu wa Shahada ya Uzamili ya Kiswahili mwenye ufaulu wa juu, akiwa na alama (GPA) ya 4.0 kwa shahada na GPA ya 4.6 (uzamili) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), ni mmoja wa vijana wa Tanzania wanaotafuta ajira au kujiajiri kupitia fani walizosomea na si kufanya shughuli nje ya taaluma.

Tofauti na malengo yake, Mgidula yuko mtaani bila ajira, hivyo kulazimika kujikita kwenye ujasiriamali wa chakula, akipika na kukiuza kupitia mitandao ya kijamii.

Mkazo wa matumizi ya Lugha ya Kiswahili na fursa zinazoambatana nazo ikiwamo kufundisha nje ya mipaka, uliwekwa zaidi kuanzia serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli.

Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa mstari wa mbele kuendeleza na kukuza Kiswahili. Mwaka jana katika Mkutano wa 36 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia, alihutubia kwa Kiswahili.

**SAFARI YAKE**


Akisimulia historia yake, anasema alihitimu shahada ya kwanza mwaka 2021 na kupata ufaulu mzuri, lakini kila anapoomba kazi hapati.

"Kwa mfano, chuo kikuu wakitangaza nafasi wanataka watu wawili au mmoja tu na unakuta sisi tumemaliza wengi, hivyo inakuwa ni bahati kupata," anasema.

Mgidula ambaye ni mtoto wa kwanza katika familia ya watoto watatu, anasimulia kuwa alipomaliza kusoma, kazi ilikuwa kupata ajira, hivyo katika kuhangaika, amewahi kufanya kazi ya kujitolea katika moja ya kampuni za magazeti nchini.

"Wakati ninaendelea na kazi ya kujitolea katika kampuni hiyo mwaka 2021, nikapata ufadhili wa kuendelea kusoma kwa hiyo nikarudi UDSM kwa masomo ya uzamili," anasema huku akibainisha kuwa amesomea kufundisha Kiswahili kwa wageni, utunzi wa vitabu, uandishi wa miswada, uhariri na uhakiki wa maandiko.

"Nilipomaliza nilitafuta kazi na nikawaza namna nitakavyotumia elimu yangu kufanya kile hasa nilichosomea. Kuna vikwazo vingi na kikubwa ni mtaji.




Ester Mgidula, akiwa katika chumba cha habari cha Nipashe, Mikocheni, Dar es Salaam, baada ya mahojiano hivi karibuni. **PICHA: RESTUTA JAMES**

Kwa hiyo nikaona nianze kupika na kuuza chakula, wakati nikitafuta ajira na mtaji wa kufanya mambo makubwa zaidi kwa nilichokisomea" anasema.

Chakula anachopika, anasema anakiuza mtandaoni (online) na wateja wake wengi huagiza ndipo hupika. Anasema alianza kazi hiyo Juni, mwaka huu, kwa mtaji wa Sh. 200,000 na hadi sasa umefikia Sh. 400,000.

Anasifu kuwa kufundisha Kiswahili kwa wageni ni kozi nzuri lakini changamoto yake ni upatikanaji wa mtaji wa kuanzisha kituo cha kufundishia somo hilo.

**AJIRA NAFASI MBILI**

Mgidula anasema nafasi za kufundisha chuo kwa mwaka zimekuwa zikitoka mbili au moja na wakiomba kufundisha sekondari, mfumo unawakataa kwa sababu hawajasoma ualimu.

"Serikali ingetengeneza sera madhubuti ya kutusaidia sisi tunaotoka vyuoni, ili kama leo nikitaka kufundisha Kiswahili nisikutane na msururu wa masharti ya kujiajiri. Tukihitimu tutambulike na kusaidiwa ili tusimame," anasema.

"Nina rafiki zangu wamesoma usimamizi wa biashara, saikolojia, masuala ya benki, wako tu mtaani kama mimi na wengine ni wamachinga Kariakoo. Naamini kuna jambo serikali yetu inapaswa kufanya ili tusikae mtaani kama hivi," anashauri.

Pia anasema elimu ya kujitegemea na ujasiriamali inatakiwa ifundishwe kuanzia shule za msingi hadi chuo kikuu. Hii itatusadia sayansi na teknolojia isituathiri sana.

Mhitimu mwingine, ambaye hakutaka jina lake litajwe gazetini, anasema alihitimu UDSM mwaka 2021 na kupata GPA ya 4.0, lakini hajapata ajira ya kile alichosomea. Anasema amefanikiwa kuajiriwa kwenye moja ya migahawa jijini Dar es Salaam, anakopika na kuhudumia wateja, tofauti na alichosomea.

**TATIZO KIMFUMO**

Aliyekuwa Mhadhiri Mwandamizi UDSM, Dk. Donath Olomi, anasema wahitimu wa chuo kikuu na wa ngazi mbalimbali, kushindwa kujiajiri ni tatizo la kimfumo linalohitaji kurekebishwa.

"Mfumo wetu haujawa na kile kitu kinaitwa meritocracy (kutambua uwezo wa mtu). Mtu mwenye GPA kubwa hawapaswi kuwa wanazunguka barabarani. Mfumo ulipaswa kuwatambua na kuwawezesha," anasema.

Dk. Olomi anasema mifumo ya ajira ilipaswa kuwatambua wahitimu wenye ufaulu wa juu na kuwapa kipaumbele, huku vyuoni na kwenye ngazi za elimu, zikiwafundisha na kuhakikisha wanafaulu kwa haki bila upendeleo.

"Mfumo wa ajira haujazingatia vizuri kuchagua watu wenye uwezo mkubwa. Hapa unazungumzia watu wachache wenye upekee. Lakini tunaangalia pia maandalizi ya jumla kwa vijana wetu kuona fursa mbalimbali ndani na nje ya nchi," anasema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Ushirika cha Wajasiriamali Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUGECO), Revocatus Kimario, anasema kuna pengo kubwa kati ya ujuzi unaotolewa chuoni na ule unaohitajika kwenye soko la ajira.

"Chuo ni kiwanda kinachozalisha bidhaa ambayo ni rasilimaliwatu, swali la kujiuliza ni je, tunazalisha kweli watu sahihi wanaohitajika sokoni? Wengi wanaotoka vyuo vikuu wana ujuzi pungufu," anasema.

**UELEWA WA CHINI**

Kimario ambaye amekuwa akilea vijana kitaaluma na kuwatafutia ajira za muda nje ya nchi, anasema wahitimu wengi wana uelewa wa kawaida na wanakosa maarifa yanayohitajika kwenye soko la ajira.

"Kuna utafiti umetoka unaonesha kwamba asilimia 69 ya wahitimu hawana uwezo wa kuchambua kitu. Hili ni tatizo kubwa mno," anasema.

Anasema vyuo vikuu vinakosa masomo ya ziada nje ya yale yaliyoainishwa kwenye kozi mahsusi, yanayoweza kumpa mhitimu maarifa yenye tija.

"Mwaka jana nilikuwa nina nafasi za kupeleka vijana 360 Ujerumani, tulishindwa kwa sababu vijana hawajui Kijerumani," anabainisha.

**UDSM YAANIKA UKWELI**

Naibu Makamu Mkuu wa UDSM (Taaluma), Prof. Bonaventure Rutinwa, anasema kila sekta nchini ina uhaba wa nguvu kazi na kinachokwamisha kuajiri ni fedha.

"Takwimu zinaonesha uhaba wa madaktari katika hospitali bingwa ni asilimia 70, lakini kuna madaktari 5,000 mtaani hawana ajira. Hapo huwezi kusema ni kwa sababu hawakuandaliwa vizuri, ni kwa sababu ya uwezo mdogo wa kuajiri na hii ndiyo changamoto kubwa hasa sekta ya umma," anasema.

Anasema uhaba wa wafanyakazi uko katika sekta zote, akisema kwamba wapo pia walimu ambao hawana ajira, wakiwamo wa masomo ya sayansi.

Prof. Rutinwa anasema asilimia 80 ya soko la ajira nchini ni kampuni ndogo na za kati, ambazo zina uwezo wa kuajiri watu watatu hadi watano, wakati kila mwaka wanafunzi 100,000 wanahitimu vyuo vikuu, UDSM ikiwa na wahitimu 15,000 kwa mwaka.

**MABORESHO MITAALA**

Prof. Rutinwa anasema chuo hicho kimeanza kufanya maboresho ya mitaala, ili kuongeza kiwango cha elimu ujuzi kwa wanafunzi.

"Mimi nimefundisha Kiswahili sekondari na baadhi ya wanafunzi wangu ni magwiji wa Kiswahili leo lakini sikuwa na cheti cha ualimu. Mambo mengine ni sera zetu. Hakuna mwalimu wa chuo kikuu mwenye cheti cha ualimu. Tatizo ni kwamba hata walimu wanahangaika," anasema.

Anashauri kwamba kunapaswa kufanyika tathmini ya uhitaji wa soko la ajira, ili kupunguza mafuriko (idadi kubwa) ya wahitimu wasio na ajira.

Anasema vyuoni wanatoa ujuzi wa aina tatu, unaohusisha uwezo kujua na kung'amua mambo, kutenda na mtizamo wa kuendelea kujifunza.

Prof. Rutinwa anashauri wazazi na walezi, kuwajengea watoto maarifa hasa nidhamu ya kazi na kuheshimu muda, ili wanapokuwa watu wazima, waweze kushirikiana na jamii inayowazunguka.

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

HABARI KITAIFA

# Watishia kutoshiriki uchaguzi wa mitaa

**Na Thobias Mwanakatwe,**
CHALINZE

WANANCHI 1,500 wa vijiji vitatu vya Kihangaiko, Msata na Pongwemsumbula katika Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze, mkoani Pwani, wametishia kutoshiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kutokana na kutolipwa fidia zao kwa zaidi ya miaka mitatu sasa.

Wakizungumza juzi katika kijiji cha Kihangaiko wakati wa kujadili suala lao, walisema Juni, 2021, walielezwa na serikali kwamba wahame katika vijiji vyao kwa ajili ya kupisha kambi ya jeshi kufanyia mazoezi.

Walisema baada ya kuelezwa hivyo tathimini ilifanyika haraka na kuahidiwa kulipwa ndani ya miezi sita, lakini hadi sasa wamekuwa wakipigwa danadana bila mafanikio.

Mwenyeviti wa kijiji kimojawapo ambaye kipindi chake cha uongozi kimeisha ambaye aliomba jina lake lisitajwe, kwa kuwa yupo kwenye kinyang'anyiro cha uchaguzi, alisema tangu walipofanyiwa tathimini wananchi walizuiliwa kutofanya shughuli zozote ikiwamo kilimo na kutojenga nyumba mpya.

Mwananchi mwingine ambaye naye aliomba asitajwe kwa kuhofia usalama wake, alisema kinachoshangaza baadhi ya vijiji ambavyo vilifanyiwa tathmini wananchi walilipwa, hali ambayo inawatia mashaka huenda kuna agenda ya siri katika suala hili.

"Suala hili tulishalifikisha kwa viongozi mbalimbali wa serikali wakiwamo wa kitaifa, lakini bado hakuna mafanikio na tumezuiliwa na jeshi hakuna kufanya chochote na ukionekana unalima au unajenga utapewa kipigo cha nguvu, " alisema mwananchi huyo.

Diwani wa Msata, Selestine Semiono, alikiri kuwa wananchi wa vijiji hicho bado hawajalipwa fidia zao kutokana na changamoto ya mwingiliano wa maeneo wakati wa kufanya tathmini.

Alisema baada ya changamoto hiyo, maofisa ardhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze walifika katika vijiji hivyo kwa ajili ya kuipatia ufumbuzi wa mwingiliano wa maeneo kati ya mwananchi na mwananchi.

Semiono alisema mchakato huo umefanyiwa kazi na sasa tathmini itafanyika upya kuanzia mwezi Desemba, 2024.

Semiono aliwaondoa wasiwasi wananchi hao kwamba serikali itawafidia baada ya tathmini kufanyika mwakani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmshauri ya Wilaya ya Chalinze, Ramadhani Possi, akizungumza na Nipashe, alisema malipo ya fidia yalikuwa ya awamu mbili ambapo awamu ya kwanza wananchi walishalipwa Sh. bilioni 9.1.

Alisema awamu ya pili ambayo itahusisha wananchi wa vijiji vya Kihangaiko, Msata na Pongwemsumbula wamesilisha maombi ya kuomba fedha kwa Mdhamini Mkuu wa Serikali.

"Tulishawasilisha maombi ya kutoa fedha za malipo ya fidia kwa mtadhimini na fedha zikitoka tutawalipa wananchi ila siwezi kusema ni lini zitaletwa hizo fedha," alisema.



Ofisa Mtendaji wa Mamlaka ya mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Isack Mgaya (katikati), akikabidhi cheti cha kuhitimu darasa la saba kwa Mwanafunzi, Elias Jacob, wakati wa mahafali ya nne ya Shule ya Msingi Glisten, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Waziri asisitiza utafiti makusanyo ya kodi kwa biashara za mtandaoni

**Na Restuta James**

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, amekiagiza Chuo cha Kodi (ITA), kufanya utafiti maalum ili kubaini namna ya kukusanya kodi ya biashara za mtandaoni.

Katika taarifa yake iliyosomwa kwa niaba yake na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Elijah Mwandumbya, wakati wa mahafali ya 17 ya ITA, Dar es Salaam juzi, Dk. Nchemba alisisitiza dhamira ya serikali kuongeza wigo wa mapato kwa kuangalia uchumi unaoendelea wa kidijitali na kwamba kuna upotevu mkubwa wa mapato unaoikabili serikali, katika sekta za biashara za mtandaoni na kimataifa.

"Tunatumai matokeo ya utafiti yatasaidia kupunguza ukwepaji wa kodi na kushughulikia mapungufu ya mapato yanayokabili serikali," alisema.

Alisema serikali inaamini kwamba utafiti wa ITA, utatoa miongozo ya wazi ya kudhibiti biashara hizo kwa ufanisi.

Aliielekeza pia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuendelea kutoa elimu ya kodi kwa wananchi ili kuongeza idadi ya walipakodi.

Aliwataka wahitimu wa ITA kuchangamkia fursa kwenye sekta za viwanda, biashara na madini, ili kujipatia kipato na kuchangia maendeleo ya nchi.

Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Chuo, Prof. Henry Chalu, alisisitiza umuhimu wa ushirikiano wa wadau ili kufikia malengo ya nchi. Prof. Chalu aliishauri sekta binafsi kuajiri wataalam wa kodi ili kurahisisha mchakato wa malipo na kupunguza makosa.

Aidha, aliwataka wahitimu hao kufanya utafiti utakaoiwezesha TRA kuongeza idadi ya walipakodi, hivyo kuisaidia nchi.

Kamishna Mkuu wa TRA, Yusuph Mwenda, alikitaka chuo hicho kuja na mifumo bunifu ya kikodi, kutambua vyanzo vipya na kushughulikia mapungufu ya ukwepaji kodi.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Isaya Jairo, alieleza namna ITA imechangia kuimarisha mifumo ya kikodi nchini na Afrika, ikiwamo kuanzisha mamlaka ya mapato Sudan Kusini.

Katika mahafali hayo, wanafunzi 417 wa fani ya uwakala wa forodha, usimamizi wa forodha na kodi, kuanzia ngazi ya cheti hadi uzamili katika kodi walitunukiwa vyeti.

Alibainisha kuwa taasisi hiyo ni kitovu cha kuendeleza mifumo ya kodi, kwa kuchanganya maarifa ya nadharia na mafunzo kwa vitendo ili kukidhi matakwa ya taaluma.

"Pamoja na uwezo wake thabiti wa mtaala na utafiti, ITA inasalia mstari wa mbele kushughulikia changamoto za kodi za Afrika," alisema.

Aliongeza kuwa maagizo ya Dk. Nchemba yanasisitiza jukumu muhimu la ITA katika kukabiliana na matatizo ya uchumi wa kidijitali.

# Nchimbi ahimiza ujuzi vitendo soko la ajira

**Na Gwamaka Alipipi**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Emmanuel Nchimbi, ameviagiza vyuo vikuu nchini kuwapa wanafunzi ujuzi wa vitendo unaohitajika katika soko la ajira na kuhakikisha elimu vinayotoa inalingana na mahitaji ya soko.

Alitoa agizo hilo jana mkoani Morogoro wakati akizungumza katika Kongamano la 24 la Mkutano wa Baraza la Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, lililohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali waliowahi kusoma katika chuo hicho.

Dk. Nchimbi alisema pengo kati ya elimu na sekta ya viwanda ni lazima lizibwe, kwamba haitoshi kwa vyuo vikuu pekee kufundisha tu nadharia bali vinapaswa kujielekeza pia katika ufundishaji wa vitendo.

Kuhusu utatuzi wa ajira, Dk. Nchimbi alisema: "Ukosefu wa ajira bado ni changamoto kubwa, lakini ni jambo linaloweza kushughulikiwa kupitia fikra za ubunifu na uvumbuzi. Lazima tuangalie mbali na mifumo ya ajira ya kawaida na kuchunguza viwanda vipya, majukwaa ya kidijitali na mwelekeo wa ajira usio wa kawaida."

Dk. Nchimbi alisema katika kuleta mapinduzi katika soko la ajira ni lazima kuendelezwe fikra za ubunifu na ustahimilivu.

"Kama wahitimu wa taasisi hii mashuhuri ya Mzumbe mmepata zana zinazohitajika kwa safari hii, ni lazima mwendeleze roho ya ujasiriamali, shauku ya uvumbuzi, na dhamira ya kujifunza maishani. Njia iliyo mbele siyo ya waoga, bali ni ya wale walio na ujasiri wa kuvunja mipaka, kuondoa vizuizi, na kubadilisha tasnia" alisema.

Kuhusu ujasiriamali, alisema ni muda mrefu taifa limekuwa likitegemea mifumo ya ajira za kitamaduni kama njia pekee ya mafanikio. Alisema ni wakati sasa wa kutafakari upya fikra hizo, kwamba mustakabali wa uchumi wa Tanzania hauko tu kwenye kujaza nafasi zilizopo katika kampuni zilizopo, bali uko katika kuunda fursa mpya, tasnia mpya, na biashara mpya.

Awali, Rais wa Baraza la Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Ludovick Utouh alisema tangu kuanzishwa kwa chuo hicho kikianza kama Taasisi ya Maendeleo Mzumbe (IDM) imezalisha wasomi wengi wanaolitumikia taifa ndani na nje ya nchi.

Alisema miongoni mwao ni Rais Samia Suluhu Hassan ambaye kupikwa kwake vyema chuoni hapo ndio matunda anayoyafanya sasa ya kuwa kiongozi bora kwa kuifanya nchi kuwa sehemu salama.

Aliwataja wengine kuwa ni Dk. Nchimbi, Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu, Balozi Ombeni Sefue ambaye mafunzo aliyoyapata chuoni hapo yamemfanya kuendelea kuaminiwa kwa kuteuliwa kwenye tume mbalimbali ikiwamo ya Haki Jinai na ya Maboresho ya Mifumo ya Kodi.

Utouh ambaye pia ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Mstaafu aliwaomba waliowahi kusoma Chuo Kikuu cha Mzumbe wakiwemo mawaziri, wabunge, mabalozi, wafanyabiashara kuendelea kuwa mabalozi wema huko walipo huku wakikumbuka kuchangia kwa chochote kwenye mfuko wa kusaidia masomo kwa wanafunzi.

Alisema kwa wahitimu wa mwaka huu wanapaswa kwenda kuitumia elimu waliyoipata kwenye maisha yao. Kadhalika aliwataka kujielekeza kwenye ujasiriamali ili kupambana na adui umaskini. Vilevile aliwataka wahitimu kuzingatia misingi mitatu pindi wanapokuwa katika ujenzi wa taifa ambayo ni uaminifu, kufanyakazi kwa bidii na juhudi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kasumba vijana kuhusu ajira mikoa ya pembezoni imepitwa na wakati

**KWA** miaka mingi, kumekuwa na kasumba iliyojengeka kwa watumishi wa umma au wafanyakazi wa sekta binafsi kukataa kwenda katika mikoa ya pembezoni pindi wanapopangiwa kwenda huko. Mikoa hiyo ni Rukwa, Kigoma, Katavi, Mtwara na Lindi. Hali hiyo pia ilizikumba baadhi ya wilaya zilizokuwa na tatizo la miundombinu au mawasiliano kama vile Simanjiro na Kiteto mkoani Manyara na Ukerewe mkoani Mwanza

Licha ya kubadilika kwa mambo ikiwamo kuboreshwa kwa miundombinu katika mikoa hiyo pamoja na kuibuliwa kwa fursa mbalimbali, bado wafanyakazi na watumishi wamekuwa wakikataa kuripoti na kufanya kazi katika maeneo hayo.

Awali, waliokuwa wakipangiwa katika mikoa hiyo miaka ya 1990 na kurudi nyuma, walikuwa na dhana kwamba wanakomolewa, hivyo kushindwa kwenda na kuamua kuacha kazi. Baadhi yao walikuwa wakiripoti kisha kuomba kuhamishwa kwa kutoa sababu mbalimbali kama vile za kifamilia au ugumu wa mazingira ya kufanya kazi.

Hata sasa, licha ya kuboreshwa kwa mazingira, hali hiyo bado inaendelea kama alivyoshangazwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu. Naibu Waziri alishangaa baada ya kubaini kuwa kuna idadi ndogo ya waombaji wa nafasi za kazi kada ya afya waliokuwa katika mikoa ya Kigoma, Katavi, Lindi na Mtwara.

Hali hiyo ni tofauti na mikoa mingine kama vile Dar es Salaam, Mwanza na Dodoma ambayo ina idadi kubwa ya waombaji kulinganisha na uhitaji. Wanaoomba kazi katika mikoa hiyo ni wachache kulinganisha na mikoa mingine.

Utaratibu wa watu kuomba kazi katika mikoa wanayotaka kufanyia kazi umeandaliwa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma badala ya ule uliozoeleka wa watu kuomba kazi na hatimaye waliofaulu usaili kupangiwa vituo.

Juni, mwaka huu, sekretarieti hiyo ilitangaza nafasi za kazi 9,483 za kada ya afya na kila mwombaji alitakiwa kuomba ajira katika mkoa ambao atafanya kazi endapo atafanikiwa kupita kwenye usaili.

Waziri Sangu alitolea mfano wa mkoa wa Kigoma, ambao mahitaji halisi ya waliotakiwa kuajiriwa katika kada ya afya yalikuwa watumishi 400 lakini waombaji walikuwa hawazidi 200. Hali hiyo pia ilikuwa katika mikoa ya Lindi, Mtwara na Katavi ambako pia idadi ikiwa ndogo kulinganisha na uhitaji.

Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, Sangu alishangazwa na uwapo wa tatizo kubwa la ajira kwa vijana nchini lakini wanashindwa kuchangamkia fursa zinapojitokeza kwa kuendekeza kasumba iliyojengeka miaka nenda rudi kwamba mikoa hiyo ya pembezoni ina mazingira magumu ya kufanya kazi na ukosefu wa baadhi ya huduma.

Licha ya kuwapo kwa hali hiyo, Naibu Waziri pia alishangazwa na tabia ya baadhi ya watumishi wanaopangiwa katika mikoa hiyo kuomba uhamisho muda mfupi baada ya kuripoti.

Hali hiyo imeiamsha serikali na kuonya kuwa haitawavumilia watumishi wa namna hiyo na kusisitiza kuwa ni lazima wafanye kazi kwa miaka mitatu na kuendelea ndipo waombe uhamisho.

Kuendelea kuwapo kwa kasumba hiyo ni jambo la kushangaza kwa sababu serikali imeboresha mazingira ya kufanya kazi katika maeneo yote ya nchi ikiwamo mikoa ya pembezoni ambayo awali ilikuwa vigumu kupatikana kwa huduma mbalimbali. Kama ni miundombinu, hivi sasa hakuna mkoa ambao haujaunganishwa na barabara ya lami. Pia kuwapo kwa miundombinu kumewezesha kuwapo kwa huduma mbalimbali kila kona ya nchi.

Ni vyema kwa vijana wanaoomba ajira, wakaachana na kasumba hiyo ambayo imejengeka katika fikra zao. Kama wahenga wasemavyo kambi popote, ni vyema vijana wanaosaka ajira wakachangamkia mikoa hiyo kwa sababu kuna uwezekano wa kupata kazi kama ilivyobainishwa na Naibu Waziri Sangu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Siasa za majitaka zisipewe nafasi kampeni uchaguzi serikali za mitaa

Na Sabato Kasika

**VIGOGO** wa vyama vya siasa wamesambaa nchi nzima, kwa ajili ya kufanya kampeni za kuungwa mkono na wananchi katika uchaguzi wa serikali za mitaa, unatarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu.

Kampeni hizo zilianza rasmi Novemba 20 na zitadumu hadi Novemba 26. Wakati huu ambao wanasiasa wanajinadi kwa wapigakura, ni vyema kuwakumbusha mambo ya kuepuka wakati wote wa kampeni.

Ikumbukwe kuwa imekuwa kama jambo la kawaida wakati wa kampeni kuona wafuasi wa vyama vya siasa wanachomeana moto bendera za vyama vyao na wengine kutukanana matusi hata ya nguoni.

Kimsingi, mtindo huo wa kuchomeana moto bendera, haina afya kwa siasa, badala yake unaongeza uhasama kwenye jambo ambalo linaweza kusababisha kuhatarisha umoja wa kitaifa.

Baadhi ya wanasiasa huwa wanawasingizia wenzao mambo mazito, kuzushiwa tuhuma mbalimbali ili mradi tu kuwapunguzia ushawishi kwa wananchi ili wawakatae.

Hivyo, siasa hizo ambazo wengine wanaziita kwa jina la 'siasa za majitaka', hazifai kuendelezwa, kwani zinaweza kusababisha mifarakano, na kujenga chuki miongoni mwa wanasiasa.

Wanasiasa kupigana vijembe kwenye majukwaa ya kampeni ni jambo la kawaida, kwani havina athari katika uchaguzi au kwa umoja wa kitaifa, lakini wanaposingiziana mambo mazito, hapo si sahihi.

Kwa wafuatiliaji wa siasa watakubaliana nami kuwa siasa za vijembe wakati wa kampeni za uchaguzi haziepukiki, kwani huwa ni sehemu ya vichombezo ambavyo vinachangia kuwavuta wapigakura.

Lakini anapotokea mwanasiasa anapanda jukwaani na kumtolea mwenzake kashfa au matusi mazito ama kumsingizia jambo fulani kwa lengo la kumshushia hadhi mbele ya jamii, ajue kuwa hilo halifai.

Hizo ndizo zinazoitwa siasa za majitaka ambazo hazitakiwi kupewa nafasi kwenye kampeni zinazoendelea, badala yake kila mgombea aeleze kile ambacho anajiandaa kuwafanyia wananchi iwapo watamchagua.

Wako wanaoamini kwamba siasa za wakati wa kampeni za uchaguzi ni mkusanyiko wa siasa nyingi, majitaka, kuelezea sera, uzushi na ukweli, ila binafsi ninatamani wanasiasa waache moja kati ya hayo.

Kuelezea sera na kusema ukweli ni mambo ya muhimu, lakini majitaka na uzushi havifai, kwa sababu havitoi mwanga au mwelekeo wa kile ambacho mgombea anataka kuwafanyia wananchi.

Watanzania wanahitaji kufahamu ni nini ambacho mgombea amejiandaa kuwafanyia kwenye kitongoji, kijiji au mtaa wao, sio kusikiliza matusi na kashfa dhidi ya wagombea wengine ili kuwatoa kwenye 'reli'.

Kwenye ngazi ya chini kuanzia kitongoji hadi mtaa, kuna kero nyingi ikiwamo ukosefu wa huduma bora za kijamii ambazo zinatakiwa kupatiwa ufumbuzi. Wagombea waeleze watakavyozitatua.

Vilevile, wanasiasa wakumbuke kuruhusu maswali ili wananchi waweze kuwauliza na kupatiwa majibu kulingana na maswali walioulizwa na sio kukwepa kuulizwa kutokana na sababu wanazojua wenyewe.

Polisi, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na wanasiasa wenyewe, ni wadau wakubwa wa uchaguzi huu, hivyo ni vyema washirikiane kuhakikisha kampeni zinakuwa za kistaarabu.

Wale ambao wamejipanga kufanya siasa za majitaka, waambiwe ukweli kuwa hazitakiwi ili wasiwachanganye wananchi, bali watangaze sera ili wapigakura waamue ni nani wamchague.

Ni wakati sasa kwa wanasiasa kujinadi majukwaani bila kuchanganya sera za vyama na vitu ambavyo vinaweza kwenda kinyume na kanuni, taratibu na sheria za uchaguzi wa serikali za mitaa.

Watanzania wa leo wanajua mambo mengi, hawadanganyiki kwa siasa zisizofaa. Hivyo, wanasiasa wajipange vizuri kuhakikisha wanatumia ushawishi usio na chembe ya siasa za majitaka.

FIKRA MBADALA

# Vyombo vya habari viwezeshwe kuwatendea haki Watanzania



Pascal Mayalla

NIMEBAHATIKA kuhudhuria mkutano wa wadau wa habari kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa uliopangwa kufanyik Novemba 27, mwaka huu.

Mkutano huo ulioandaliwa na Wizara ya Habari, Teknonojia ya Habari na Mawasiliano, ulipokea mada mbalimbali kuhusu wajibu wa vyombo vya habari kwenye uchaguzi. Moja ya mada hizo ni wajibu wa vyombo vya utangazaji kwenye uchaguzi, iliyowasilishwa na Mhandisi Andrew Kisaka kutoka M<amlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Vyombo vya utangazaji vinatakiwa kutoa elimu kwa mpigakura, kufahamisha umma mwenendo wa kampeini za vyama vya siasa, kuripoti hali halisi siku ya kupiga kura na kutangaza matokeo.

Malengo ya kanuni hizi ni kuweka mizania ya matangazo ya vyama vya siasa wakati wa uchaguzi, kuhamasisha weledi na maadili ya utangazaji, kuhamasisha uwazi, mizani na kutobagua kundi lolote katika jamii na kuhakikisha kuwa vyombo vya utangazaji haviegemei upande wowote.

Kanuni hizi zinaelekeza katika kuripoti habari za uchaguzi,utangazajiwa habari zote wakati wa uchaguzi wa vyama vya siasa unaripotiwa na kuwasilishwa bila upendeleo na kwa uadilifu bila kuonyesha mtazamo binafsi wa mtangazaji. Vyombo vya Utangazaji vinapaswa kutoa haki sawa kwa vyama vyote bila upendeleo na kwa uwiano usawa, kwa usahihi na kuripoti matukio ya kisiasa kwa uadilifu na weledi bila upendeleo.

Mchakato mzima wa uchaguzi uazimie kusisitiza umuhimu wa uchaguzi na kuhamasisha ushiriki wa wananchi wote katika mchakato wa uchaguzi; na katika kipindi cha uchaguzi, habari zinalenga masuala yanayowanufaisha wananchi hususani sera za vyama na mikakati waliojiekea kama watapewa nafasi ya kuongoza.

Uwasilishaji wa vipindi vya uchaguzi unapaswa kuwa unaendana na sera, sheria na Kanuni zinazoongoza utendaji kazi wa vyombo vya habari vya kielektroniki. Usiwe na upotoshaji wa taarifa binafsi au usingiziaji wa mgombea yeyote au mtu mwingine, au maoni yoyote yasiyofaa juu ya sifa njemazamtuyeyote; hauhusishi maoni ya kisiasa yaliyojengeka katika ubaguzi wa kimbari, rangi, ulemavu, dini, imani, jinsia au eneo analotoka mtu

Aidha, vipindi havitahusisha lugha yoyote ya kukashfu, uvunjifu wa sheria au lughayakukufuru aulugha yoyote inayoweza kusababisha vurugu au uchochezi wa maasi; vipindi havitahusisha utoaji wa maoni yoyote yanayoweza kuumiza hisia za mtu yeyote kutokana na jinsia yake, jinsi, mbari, rangi, tabaka, imani au eneo analotoka, matangazo ya chama cha siasa yatakuwa ni yale tu ambayo vyama vinataka kunadi sera zake, programu na malengo yake.

Kanuni hizi zimetoa wajibu wa kutangaza bure habari na vipindi vya uchaguzi kwa vyombo vya utangazaji vya umma pekee, yaani public broadcasting stations, kwa maana hiyo, hii maana yake ni Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) pekee.

Nikiwa mwandaaji wa maudhui, kupitia kampuni yangu ya PPR, nimeandaa maudhui ya elimu kwa umma kupitia vipindi sita vya televisheni na sita vya redio na kuviwasilisha TBC na kuwanakili TCRA.

Ili vyombo vya habari vyote viwatendee haki Watanzania wakati wa uchaguzi, hatua ya kwanza ni kuwezeshwa. Japo jukumu la kutangaza bure habari ni jukumu la vyombo vyote vya habari, jukumu la kutangaza vipindi vya bure limeachwa kwa vyombo vya habari vya umma pekee na hakuna kipengele chochote kinachozungumzia uwezeshaji wa vyombo vya habari kutumiza wajibu.

Nilizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa TBC, Dk. Ayub Rioba, na baada tu ya kumweleza kuhusu vipindi hivyo, alikubali TBC kuvipokea na kunielekeza kuvikabidhi kwa mkuu wa vipindi ili kuangalia maudhui na wakijiridhisha vitarushwa hewani.

Kwanza nitoe pongezi kwa Mkurugenzi Mkuu wa TBC kwa kunipokea na kunikubalia leta vipindi tuviangalie. Hii ni hatua kubwa ya kustahili pongeza hata kama mwisho wa siku, vipindi havitarushwa. Ile nia njema tu ya ruhusa ya TBC kupokea vipindi ni jambo jema.

Pia nitoe pongezi kwa Mkuu wa Vipindi TBC, Happiness Ngasala, kunipokea na kuvipokea vipindi vyangu lakini pia ili TBC itimize majukumu yake kikamilifu, hata TBC inatakiwa kuwezeshwa, ili kutoa hiyo muda wa kurusha matangazo au vipindi bure kwa elimu kwa umma na kwa vyama vya siasa.

Uwezeshaji huu usiishie kwa TBC tu. Kanuni inaelekeza vituo binafsi vya utangazaji, kupanga bei rafiki kwa vyama vyote vyenye uwezo wa kulipia, virushe vipindi vyao.

Kwa vile hali za uchumi wa vyama hazifanani, kuna vyama vina nguvu za kiuchumi kumudu kulipia vipindi vyao na kuna vyama, haswa ambavyo havipati ruzuku, hali zao ni taabani, haviwezi kumudu hata gharama za kuandaa maudhui, licha ya gharama za kuvilipia, hivyo matangazo ya vipindi yatakuwa ya vyama tajiri na vyenye uwezo pekee.

Watanzania wana haki ya kusikia sera za vyama vyote bila ubaguzi. Serikali , mamlaka ya mawasiliano na wadau wabuni njia za kuziwezesha vyombo vyote vya umma na binafsi wakati wa uchaguzi, Kutenda haki sawa kwa vyama vyote na kuwapa Watanzania haki ya kusikia sera za vyama vyote bure bila vyama kulazimika kulipia bila TBC kubebeshwa mzigo wote wa kurusha vipindi vya bure bila kuwezeshwa.

Nawatakia Watanzania, uchaguzi mwema wa serikali za mitaa.

Mungu Ibariki Tanzania.

**Paskali. +255 754 270403**

KONA YA AFYA

# Zijue dalili za mtu mwenye sukari



Na Dk. Mabula Budodi

HIYO siku naikumbuka sana. Ni kama jana tu kwangu maana donda lilianza kama utani. Kilianza kimchubuko kidogo ambacho kilisababishwa na kujikwaa kwenye kimti mguuni. Hata sikuchukulia maanani maana nilijua itakuwa kama siku zote ni kimchubuko cha kawaida kitapona ndani ya siku moja au mbili, hivyo maisha yakaendelea kama siku zote.

"Lakini haikuwa hivyo baada ya siku ya kwanza, niliona dalili ya kuanza kupona, lakini kadiri siku zilivyoenda kilianza kutoa maji maji na kuanza kuchimbika. Nilishangaa na kujiuliza maswali mengi kwa nini inakuwa hivi?

"Nilijijibu moyoni tu labda kwa sababu sikupata kuchoma sindano ya tetanasi ndiyo mana kimekuwa kikubwa. Nilikwenda zahanati na kuomba kuchoma sindano ya tetanasi na kisha kusafisha kidonda na kuondoka huku nikiwa na matumaini makubwa kwamba sasa nitakuwa salama."

Hiyo ni kauli ya mgonjwa ambaye alipata tatizo ambalo hakujua chanzo ni nini. Anasema tokea hapo aliona dalili ya ongezeko la kidonda hicho. Hali hiyo, anasema ilianza kumfanya awaze kweli na hata kuanza kuhisi vitu vingi kichwani.

Anasema kadiri muda ulivyosonga, aliona hali ikiendelea hivyo na siku moja alikutana na rafiki yake amabaye ana kisukari na kumshauri kwamba anasema labda anaweza kuwa na tatizo la sukari, hivyo inabidi akapime. Alimkatalia na kusema kwao hakuna suala la sukari. Aliendelea kusafisha kidonda na kutumia dawa za kienyeji kwenye kutibu kidonda.

"Ni kwa namna gani nilikuwa na uelewa mdogo sana kuhusu ugonjwa wa sukari, kadiri siku zilivyoendelea sikupata ahueni hata kidogo zaidi ya kuendelea kuoza mguu kutokana na janga hilo. Niliogopa kweli na kujiuliza tena maswali mengi yasiyo na majibu kichwani.

"Niliamua kufuata ushauri wa rafiki yangu aliyenishauri siku nyingi zilizopita na kutembelea hospitali, tena hospitali kubwa. Nilikutana na daktari aliyenisikiliza na kuniuliza maswali kadhaa mojawapo likiwa huwa nina matatizo ya sukari na nilishawahi kupima. Nilijibu kwa hofu kuwa hapana sijawahi kupima sukari.

"Nilijawa hofu maana nilishasikia taarifa nyingi za watu wa sukari kuhusu kutokula vyakula karibia vyote ninavyovipenda na kunywa dawa nyingi zisizo na hesabu, anabainisha.

Baada ya maelezo hayo, anasema daktari alimwambia kuwa kama alivyomweleza kuna uwezekano mkubwa wa kuwa na tatizo la sukari, hivyo wanaweza kupima kiwango cha sukari kwa wakati huo, sukari ya kufunga bila kula chakula ndani ya saa nane na kiwango cha sukari ya ndani ya miezi mitatu ili kupata uhalisia zaidi juu ya kiwango cha tatizo.

Baada ya majibu kutoka aliambiwa sukari na inasoma iko 28 kwenye kipimo na inaashiria kwamba miezi mitatu isomeke 13 na wanatarajia iwe chini ya 6.5% kwa mtu ambae hana matatizo ya sukari.

"Hivyo kama ukiwa unasukari ya kiwango cha kawaida inayotakiwa itasaidia kwenye kupona kwa kidonda hicho. Akasema sasa tutaanza matibabu, nitakuelekeza namna ya kuishi na sukari," anasimulia.

Anasema masharti na maelekezo aliyopewa hayakuwa magumu kufuata si kama alivyokuwa anasikia kwa watu wa mtaani na vitisho kuhusu sukari. Ndani ya miezi miwili mpaka mitatu kidonda kilikuwa kimepona kabisa na aliendelea na maisha mengine kama kawaida huku akihudhuria kiliniki ya sukari kila mwezi bila kuacha.

**HALI DUNIANI**

Inakadiriwa kuwa watu milioni 422 wanaishi na ugonjwa wa kisukari duniani kote, ikiwa ni mara nne zaidi ya miaka 40 iliyopita kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

Kisukari ni ugonjwa unaoelezewa na kuwa na kiwango kikubwa cha sukari mwilini kwa sababu ya mwili kutokutumia insulini vizuri au kutokuzalisha insulini ya kumeng'enya sukari mwilini.

Kuna aina kuu mbili za kisukari. Kisukari aina ya kwanza ambacho hupatikana kwa Watoto na vijana huanzia umri mdogo na husababishwa zaidi na mwili kutokuzalisha insulini ya kutosha.

Sukari ya aina ya pili huanza katika umri mkubwa, yaani kwa watu wazima na husababishwa na mwili kutokutumia insulini iliyoko mwilini.

Dalili za ugonjwa wa kisukari mwilini ni kukojoa mara kwa mara bila hata kunywa maji, kiu iliyopitiliza hata mtu akitaka kunywa maji muda si mwingi, kupungua uzito bila sababu isiyoeleweka, kuwa na njaa iliyopitiliza hata baada ya kula mda mfupi, kuchoka sana mwili, kutokuona vizuri, kutokupona vidonda mapema na hata pia kuumwa mara kwa mara.

MATIBABU YAKE

Matibabu ya kisukari huhusisha kubadili mfumo wa maisha na matumizi ya dawa, yaani kufanya mazoezi, kupima sukari mara kwa mara, kula vizuri majani na mboga zaidi na kupunguza wanga na kupunguza msongo wa mawazo.

Madhara ya sukari huweza kutokea kwenye moyo, figo, macho na hata kutokuweza kuhudumia familia kwa wanaume na hata mwili mzima kudhoofika. Jambo la msingi ni kuzingatia matibabu, kufuatilia afya kwa kupima hasa kwa mtu ambaye hajagundulika na kuwa na tatizo la sukari.

Ni muhimu kufuata masharti na ushauri wa daktari.

- Dk. Budodi ni daktari **wa tiba ya binadamu anapatikana kwa simu namba 0710 980096 na baruapepe mabulabudodi@gmail.com**

# Walimu wagoma kufundisha kisa mishahara

**Na Grace Mwakalinga**

WALIMU wa Shule ya Sekondari ya Jumuiya ya Wazazi (CCM) Meta, iliyoko katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wamegoma kufundisha na kusimamia mitihani, kwa madai ya kutolipwa mishahara yao kwa zaidi ya miaka mitatu.

Wakizungumza na waandishi wa habari juzi walimu hao walisema, wamechoshwa na hali ngumu ya maisha inayowakabili kutokana na malimbikizo hayo, huku wakiitaka Jumuiya ya Wazazi ya CCM kuwalipa stahiki zao.

Mwalimu Seth Mwakilima, alisema wanashindwa kuelewa sababu ya hali hiyo, akidai sio wao tu, bali hata taasisi nyingine zinazomilikiwa na chama hicho hazijapatiwa stahiki zao.

Alisema wanachohitaji kwa sasa ni mishahara yao na fedha za kujikimu, si ahadi nyingine yoyote.

"Sisi walimu wa Shule ya Meta, tunahitaji kulipwa stahiki zetu, tumevumilia kwa muda mrefu, lakini sasa tumefikia mwisho.

Mwalimu Tabu Kahindi alisema maisha yao yamekuwa magumu ambapo kwenda kazini imekuwa ngumu zaidi kwa sababu ya kukosa nauli.

Alitolea mfano tukio alilokumbana nalo hivi karibuni ambapo aliumia akiwa kazini, lakini hajapata matibabu kwa sababu hana fedha za kutibiwa.

Mwalimu Tito Ngailo alisema hawana fedha za kulipa kodi wala ankara za maji na umeme, hali inayozidi kuwaweka katika mazingira magumu, huku familia zao zikitewagemea.

Mwalimu wa Taaluma shuleni hapo, Christopher Nswima, alisema hali ya kitaaluma kwa wanafunzi haikuwa mbaya hapo awali kwa sababu walijitahidi kufundisha kwa mshikamano.

Alisema ndani ya wiki hii, walimu walishindwa kuendelea kutokana na kuchoka kuvumilia hali ya kutolipwa mishahara, jambo ambalo limeanza kuathiri mitihani inayoendelea.

Katibu wa CCM Mkoa wa Mbeya, Lengai Akyoo, alikiri kuwapo kwa changamoto hiyo na kueleza hatua zilizochukuliwa kutafuta ufumbuzi.

Alisema suala hilo tayari limeripotiwa ngazi ya taifa, na timu imetumwa kushughulikia jambo hilo.

Alisema timu hiyo tayari ipo mkoani humo na itakapokamilisha kazi yake, itawasilisha ripoti kwa Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Emmanuel Nchimbi.



Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande (kulia), akimtunuku mmoja wa wahitimu wa shahada mbalimbali, wakati wa Mahafali ya 10 ya Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC), jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: WF**

# Wafanyakazi wa kujitolea Marekani waapishwa

**Na Jenifer Gilla**

WAFANYAKAZI 25 wa kutoka nchini Marekani chini ya Mtandao wa Kimataifa wa Wafanyakazi wa Kujitolea (PEACECORPS) wameapishwa kwa ajili ya kuanza kazi hiyo nchini.

Akizungumza katika hafla fupi ya uapisho mapema wiki hii jijini Tanga, Balozi wa Marekani Nchini, Michael Battle, alisema wafanyakazi hao wapo tayari kuihudumia jamii ya Tanzania baada ya kupitia mafunzo ya wiki 12 ya kina.

Alisema mafunzo waliyopitia wafanyakazi hao ni lugha ya Kiswahili, utamaduni, ulinzi na usalama, afya na ujuzi mahsusi wa sekta katika kukabili na kutoa ujuzi kwa jamii.

Balozi alisema wafanyakazi hao wataishi na kufanyakazi kwa miaka miwili katika mikoa ya Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Njombe na Zanzibar wakifundisha masomo ya hisabati na sayansi, eneo la afya ya jamii, kilimo endelevu kinachohusisha ukuzaji wa ustahimilivu wa hali ya hewa katika shule za sekondari.

Aliwaeleza wafanyakazi hao kuziwezesha na kuziongoza jamii kufahamu vipaumbele na mahitaji yao, ili washirikiane kwa pamoja kutafuta ufumbuzi endelevu wa matatizo yao.

"Kazi mnayofanya hapa mkishirikiana na wafanyakazi wenzenu wa Kitanzania na majirani inaweza kubadilisha maisha. Muwe na ndoto kubwa, lakini kumbukeni kutokubaki na ndoto hiyo wenyewe," alisema.

Alisema wafanyakazi hao wataungana na wenzao 3,200 katika kuenzi urithi ulioachwa na Mwalimu Julius Nyerere na Rais John Kennedy wa kujitoa kwa ajili ya amani na urafiki duniani tangu ilipoanza programu ilipoanza mwaka 1961.

Mkurugenzi Mkazi wa Peace Corps Tanzania, Stephanie Joseph de Goes, alisema kinachofanya shirika hilo kuwa la kipekee ni mbinu yake ya kuleta maendeleo ya watu ikiwa ni kusimamia kwenye msingi wa ubia imara ulioanza zaidi ya miaka sitini iliyopita.

Aliishukuru Tanzania kwa msaada, ushirikiano wanaoutoa kwako, na kuwa imani walionayo kwao inawawezesha kuhudumu kikamilifu pande zote za nchi hiyo.

"Ni maendeleo yenye msingi wake kwa watu, yanayozingatia kujenga uhusiano mzuri na yanayopewa msukumo na mahitaji na matamanio ya jamii. Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa wabia wetu serikali ya Tanzania," alisema.

# Watakwimu wapewa somo viashiria vya kiuchumi EAC

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Fedha, Hamad Chande (Mb), amewataka wadau wote wa takwimu rasmi kushirikiana na serikali katika kukokotoa viashiria vya maendeleo.

Amewataka kutathmini hatua zilizopigwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa inayoisha mwaka 2025 na hatua zilizopigwa katika Malengo ya Maendeleo Endelevu yanayoisha mwaka 2030.

Chande alitoa rai hiyo wakati wa Mahafali ya 10 ya Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC) yaliyofanyika Dar es Salaam.

Alisema lengo la wadau wa takwimu rasmi liwe kuhakikisha takwimu zinakuwa rahisi kutumika katika kupanga mipango ya kukuza uchumi, kuboresha huduma za jamii, kutunza mazingira na kupunguza umasikini bila kuwaacha wengine nje.

"Ukuaji wa uchumi wa mmoja mmoja na ubora wa hali ya maisha na mazingira unatarijia mipango bora inayopimika kwa takwimu rasmi, hivyo katika mahafali haya. Nakipongeza chuo kwa kuzalisha wataalam mbalimbali katika tasnia pana ya takwimu rasmi na nawasihi kutimiza majukumu yenu kwa weledi ndani ya taifa, Afrika na duniani kote," alisema.

Kuhusu matumizi ya kidigitali katika masuala ya takwimu, Chande alisema serikali tayari imeandaa mazingira kwa wananchi wake na wafanyabiashara kumudu mabadiliko ya kidijitali kwa kuweka anwani za makazi za kidijitali pamoja na maboresho ya teknolojia ya mawasiliano yanayorahisisha upatikani wa taarifa za sensa na tafiti ndogo katika ngazi ya vitongoji, mitaa na shehia.

Chande alisema kwa wadau wa sekta binafsi hususani rika la vijana, walio masomoni, wahitimu na walioko makazini, wanatakiwa kuwekeza zaidi katika sekta ya ubunifu wa mifumo ya biashara dijitali na kilimo cha kisasa.

Pia aliishukuru Kamisheni ya Uchumi Afrika ya Umoja wa Mataifa (UNECA), mabalozi, maofisa wakazi wa mashirika ya Umoja wa Mataifa, washirika wa maendeleo, wakurugenzi wakuu wa ofisi za taifa za takwimu za nchi wanachama wa chuo na wadau wengine wanaoshirikiana na chuo kwa kuwa kunawezesha kusukuma mbele gurudumu la maendeleo kitaifa, kikanda na kimataifa.

# MAISHA

NOVEMBA 24, 2024

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




HARUSI

Ukurasa 12





# Tanki vazi lenye mambo mengi

Ukurasa 13

# WATOTO

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA



| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | 3 | 2 | 4 |
| 4 | 2 | 3 | 1 |
| 2 | 4 | 1 | 3 |
| 3 | 1 | 4 | 2 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| G | A | B | O | N | ■ |
| ■ | N | ■ | M | ■ | J |
| ■ | G | H | A | N | A |
| ■ | O | ■ | N | ■ | P |
| ■ | L | ■ | ■ | ■ | A |
| T | A | I | W | A | N |


## FUMBO TOTO

Katika fumbo hili, herufi nyingi zimeshajazwa, ila halijakamilika. Hivyo basi, tumia herufi zifuatazo kujaza fumbo hili, kila herufi utakayotumia usiirudie tena:

E E B H M A O I B

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| A | ■ | S | ■ | |
| U | | E | M | |
| ■ | ■ | | ■ | I |
| U | ■ | | ■ | ■ |
| J | | M | | |
| | ■ | U | ■ | A |

## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI





## AMSHA AKILI

HAYA WADOGO ZANGU, TUENDELEE NA AMSHA AKILI IITWAYO SUDOKU. JAZA NAMBA MOJA MPAKA NNE KWA KILA MSTARI IWE KUTOKA CHINI MPAKA JUU AMA KUSHOTO KWENDA KULIA. HAKIKISHA NAMBA ZINAZOFANANA HAZIGONGANI KATIKA MSTARI MMOJA. KAZI KWAKO!

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4 | | | |
| 2 | | 4 | 3 |
| 3 | | | |
| 1 | | | |

## CHEKA



Alichokifanya daktari

TOFAUTI ya wazazi wa hapa nchini mtoto wa Tanzania na sehemu zingine wakati anapolala inakuwa kama hivi.

Marekani mtoto anapokwenda kulala huagwa na wazazi wake “usiku mwema mwanangu”

Uingereza wazazi wanamuaga mtoto wao “Pata njozi njema mwanetu”

Hispania anapokwenda kulala wazazi humuambia “usiku mwema mpendwa wetu”

Tanzania mtoto anapotaka kulala wazazi utawasikia “Kesho uamke mapema, hatutaki kusikia umechelewa na hela ya mihogo utaikuta mezani”

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Uhusiano ndoto za usiku na matatizo ya watu wengi

NAKUKARIBISHA tena msomaji wangu tuendelee kuangazia ndoto unazoota usiku. Tayari tumeangalia maana ya ndoto na aina zake. Pia sababu za kuota ndoto na shuhuda zinavyotesa na kuua watu.

Leo tuchambue uhusiano kati ya ndoto na matatizo ya watu. Moja kati ya chanzo cha matatizo ya watu wengi ni ndoto wanazoota. Kupitia ndoto unaweza ukaibiwa vitu vyako vizuri. Au unaweza kupandikizwa vitu kama magonjwa, vifo na unaweza kufanywa msukule!

Hebu msomaji wangu nikupitishe kwenye baadhi ya ndoto wanazoota watu mbalimbali zikawasababishia matatizo. Watu wengi wanapuuzia ndoto na baadaye kile walichokiota kikitokea wanajilaumu kinapotokea vile vile kama walivyoota.

Dada mmoja aitwaye Juliana, katika moja ya mikutano ya injili alitoka mbele na kueleza ndoto anazoota. Akasema hivi; Mimi huwa naota nafanya tendo la ndoa na mbuzi, na nikiamka asubuhi najikuta nimechafuka sehemu za siri huku mwili wangu ukinuka harufu ya mbuzi (kinyesi cha mbuzi).

Ndoto hii imenisumbua kwa muda mrefu na mara zote nikishaiota tu, matatizo yanaanza ndani ya nyumba yangu. Kwanza ninaanza kugombana na kutukanana na mume wangu bila sababu ya msingi. Na kingine ninahisi maumivu makali ya tumbo.

Hapa nilipo nimeishi na mume wangu miaka mitano lakini sijafanikiwa kupata mtoto. Nahitaji msaada niondokane na kadhia hii. Anamaliza maelezo yake.

Wakati wa maombezi iligundulika kuwa ameolewa na mizimu ambayo hujigeuza mbuzi na kumwingilia wakati wa usiku. Hata hivyo, alifunguliwa kabisa na sasa ana mtoto wa kike!

Ndoto nyingine, yuko dada mmoja aitwaye Leah, aliota anachomwa sindano na mtu na alipoamka akashangaa kuona mwili wake una alama kama za kitu chenye ncha kali kimemchoma.

Baada ya mwezi afya yake ilianza kuzorota na alipoenda kupima iligundulika kuwa ana virusi vya Ukimwi. Hali hiyo ilimshtua sana kwani hakuwahi kushiriki tendo la ndoa na mwanaume yoyote (alikuwa bikira).

Alipoombewa, roho za kipepo zilianza kuongea na kusema; "Ni sisi tulikuja kitandani kwake tukamchoma sindano yenye virusi vya Ukimwi. Tunataka tumuue, hatutaki aolewe na Frank". Kumbe chanzo cha ugonjwa kilianzia kwenye ndoto.

Kaka Jofrey, alifukuzwa kazi baada ya kuota amepoteza vyeti vyake vya shule na vitambulisho vyake vya kazi. Dada Maria yeye aliteswa na roho ya utasa kwa miaka 13. Baada ya kuombewa roho hiyo ilimwachia na sasa ni mjamzito.

Kwa maelezo yake akasema, "Tokea nimeolewa haiwezi kupita wiki sijaota kuwa nimezaa mbwa wengi na kuwanyonyesha. Hali hii imekuwa ikinitokea mara kwa mara".

Wakati wa maombezi zililipuka roho na sauti ikatoka kinywani mwake ikisema; Huyu ni mali yetu na hao anaowaota ni watoto wetu. Hawezi kuzaa kwa hali ya kawaida kwani ni mke wetu na sisi hatuchangii mke". Hayo mapepo yalimwachia na sasa ni mjamzito.

Dada mmoja naye aliota nyoka anamgonga kwenye mkono. Alipoamka alishangaa kuona mkono umevimba na una maumivu makali sana. Baada ya siku chache alipoenda kupima hospitali walimwambia ana kansa kwenye huo mkono.

Kwa kuwa alijua chanzo cha tatizo alikimbilia kanisani. Baada ya maombezi maumivu yalikoma.

**Baada ya mwezi afya yake ilianza kuzorota na alipoenda kupima iligundulika kuwa ana virusi vya Ukimwi. Hali hiyo ilimshtua sana kwani hakuwahi kushiriki tendo la ndoa na mwanaume yoyote (alikuwa bikira).**

Aliporudi hospitali kupima madaktari walishangaa sana walipoona vipimo havina chembechembe za kansa. Ndoto hii inatufundisha kama dada huyu angepuuzia ile ndoto huenda angekufa kwa kansa hiyo ya kipepo.

Kaka Ezekiel alikuwa na tatizo sugu la uchumi. Akasema kila alichokuwa akifanya kilikuwa kinaharibika. Alipoulizwa na mtumishi wa Mungu aeleze aina za ndoto anazoota alisema;-

"Mara nyingi huwa naota nipo makaburini napalilia makaburi ya nyumbani kwetu. Wakati mwingine naota naongea na babu na bibi waliokufa. Wakati mwingine nakula vyakula nikiwa na hao ndugu zangu waliokwisha kufa na nikiamka asubuhi nahisi nimeshiba.

Wakati wa maombezi ilifichuka kuwa ameunganishwa na roho za mauti ndio maana kila anachokifanya hakifanikiwi. Wengi wanaota ndoto za aina hii wanachukulia kawaida. Zinduka ndugu tafuta watumishi wa Mungu wakuombee hizo roho zikuachie, maisha yaendelee.

Bila shaka msomaji wangu umejifunza kitu kuhusiana na ndoto za wenzetu hapo juu. Je, wewe unaota ndoto gani. ***Tuma ndoto inayokuogopesha kwa ujumbe mfupi kwenye namba 0715268581 usaidiwe. Namba pia ipo WhatsApp.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Kampeni hizi zisigeuzwe eneo la vita kuumiza wengine

KILA mtu aitii mamlaka iliyo kuu, kwa maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu; na ile iliyopo imeamriwa na Mungu (Warumi 13:1-7).

Kama ndiyo, hawa tunaotaka kuwachagua katika uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji kwenye uchaguzi wa juma lijalo, ni wazi wanatokana na andiko langu katika aya ya kwanza.

Lakini hawa ni lazima wapatikane kihalali, kwa njia halali na kupita katika mifumo yote halali kikatiba.

Iko wazi kwamba, maendeleo ya kweli ni ya watu na yanaletwa na watu. Watu lazima wawe chanzo na lengo la maendeleo. Watu ndio wenye mamlaka na maamuzi ya maendeleo yao.

Hili linawezekana pale tu unapokuwa na viongozi wazuri na waliochaguliwa kwa haki.

Ili kufanikisha uchaguzi, ni lazima kuwe na mfumo wa wazi, wa haki na uwajibikaji katika kusimamia uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa.

Wameeleza kuwa, tangu mchakato wa uchaguzi wa serikali za mitaa kwa mwaka huu 2024 uanze, wananchi wamekuwa wakilalamikia utaratibu wake kutotendewa haki.

Kwa mujibu wa Ibara ya 146 (1) ya Katiba ya Tanzania, lengo la Serikali za Mitaa ni kukabidhi madaraka kwa wananchi.

Kampeni za uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji, zinafanyika kati ya Novemba 20 hadi 26 mwaka huu nchini kote, ili kupisha uchaguzi utakaofanyika Novemba 27.

Kama kaulimbiu ya uchaguzi huo isemavyo, 'Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi, Jitokeze Kushiriki Uchaguzi.' Nashauri vyama 18 vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi huu, kuheshimu kanuni za au taratibu zilizowekwa.

Tunawataka Watanzania kufanya maamuzi sahihi leo kwa maendeleo ya kesho. Kila kura itaamua mustakabali wa jamii.

Ni vyema tukachagua viongozi wenye maadili, mipango na uwezo wa kutatua changamoto za wananchi wenzao.

Lakini miongoni mwa mambo ya kuzingatia kwa viongozi wa vyama vya siasa, ni yale yanayobishaniwa na kuzua vurugu katika kila uchaguzi.

Mosi, kwa mujibu wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI, mikutano ya kampeni za uchaguzi, zitaanza saa 2:00 asubuhi na zitamalizika saa 12:00 jioni ya kila siku ya kampeni.

Pili,cChama cha siasa kinachoshiriki uchaguzi kitawasilisha ratiba yake ya mikutano ya kampeni za uchaguzi kwa msimamizi wa uchaguzi kabla ya kuanza kwa kampeni.

Tatu, msimamizi wa kampeni ataunganisha ratiba ya kampeni za uchaguzi kwa kushirikisha vyama vya siasa vitakavyoshiriki uchaguzi.

Nne, msimamizi wa uchaguzi atawasilisha ratiba ya kampeni za uchaguzi kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi Wilaya husika (OCD), ambaye atakuwa na wajibu wa kuisimamia ili kuhakikisha ulinzi na usalama unakuwepo kwa kipindi chote cha kampeni. Aidha, atavipa vyama vyote vya sziasa nakala ya ratiba hiyo.

Tano, ratiba ya kampeni itakayowasilishwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya, itakuwa ni taarifa rasmi ya mikutano ya kampeni.

Kwa nini haya ndiyo mambo muhimu ya kuzingatia ili kulinda amani yetu iliyopo ni kwa sababu tunataka kuimarisha uwajibikaji na uwazi katika serikali za mitaa.

Vilevile, tunataka kuchochea maendeleo endelevu katika ngazi ya mitaa na kuhamasisha ushiriki wa jamii katika uamuzi wa maendeleo.

Kadhalika, tunataka kudumisha Amani na usalama katika jamii na kukuza demokrasia na haki za wananchi.

Jambo linguine ni kujenga utamaduni wa kuwa na uongozi bora. Kwa hiyo hakikisha unashiriki kikamilifu katika uchaguzi huu, kwa sababu uamuzi sahihi, kura sahihi, ndiyo msingi wa maendeleo tunayoyahitaji.

Kwa mujibu wa TAMISEMI-maeneo ya utawala yatakayofanya uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu, ni vijiji 12,280, mitaa 4,264 na vitongoji 63,886.

Katika uchaguzi huo, Watanzania wenye sifa watagombea kuomba kuchaguliwa kwenye nafasi 332,584 za serikali za mitaa.

Vijiji vitakavyofanya uchaguzi huo, ni vijiji 12,280 kutoka vijiji 12,333 vilivyotangazwa hapo awali.

Imo mitaa 4,264 tofauti na mitaa 4,269 iliyotangazwa hapo awali, na vitongoji 63,886 ukilinganisha na vitongiji 64,274 vilivyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali, Tangazo Namba 796 na 797, yote ya tarehe 06 Septemba, 2024.

**Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

# HARUSI



Unaweza kusema ni tukio la kushangaza, baada ya kufanyika sherehe ya kipekee ya kuwaaga kwa Veraisha na Paschazia ambao walifunga ndoa kwa wanaume tofauti jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MC GARAB**

# MITINDO

Na Moshi Lusonzo





# Tanki vazi lenye mambo mengi

VAZI la tanki lenye kofia limebuniwa maalumu kwa ajili ya mazoezi, lakini watu wengi wamegeuza kama nguo ya kutokea nyakati za jioni.

Tanki ya kofia ni nguo iliyoundwa kwa kitambaa laini na kinachonyooshwa, chepesi na kinachoweza kupumua na kinachonyonya jasho haraka.

Vazi hili linasifika kwa kuwa na muundo wa kipekee usio na mikono na kuonyesha vyema misuli ya mikono.

Sifa nyingine ya nguo hii ni kuufanya mwili kuwa baridi na mkavu mara unapomaliza kufanya mzoezi au michezo.

Sehemu ya juu ya tanki imeunganishwa na kofia yenye muundo mzuri ulioambatana na kamba inayoweza kurekebishwa.

Vazi la tanki limetengenezwa likiwa na rangi za kupendeza na kumfanya mtu kuonekana vyema akiwa katika mwelekeo wowote.

Ni jambo la kufurahisha kwamba vazi la tanki linavaliwa nyakati zote za kiangazi, mvua na baridi pale unapokwenda kwenye mazoezi ya viungo, siha, kujenga mwili, kuinua vitu vizito, kukimbia, kucheza mpira wa vikapu na shughuli zingine za nje.

## UREMBO

Na Mary Geofrey

# ONDOKANA NA UZEE

MAKOVU yanayotokana na uzee kitaalam hujulikana kama 'liver spots' na huwa madoa mekundu au hudhurungi kwenye ngozi, ambayo hutokea kwenye uso, mikono na shingo.

Katika kesi nyingi, madoa haya huwa yanaongezeka kutokana na kupigwa na miale ya jua.

Tiba muhimu za nyumbani zinaleta matokeo mazuri kupunguza makovu ya uzee.

**Juisi ya ndimu**

Ndimu ni tiba nzuri ya kutibu makovu ya uzee kwa kutumia juisi yake.

Chukua juisi ya ndimu na upake moja kwa moja kwenye makovu ya uzee.

Ikiwa juisi ni kali sana, unaweza kuichanganya na maziwa ya mtindi na kisha kuipaka kwenye uso.

Mtindi utaacha ngozi yako laini na juisi ya ndimu itasaidia kufifisha makovu ya uzee.

Fanya zoezi hili kila siku kwa wiki mbili mpaka mwezi kupata matokeo mazuri.

Mafuta ya Mbono

Inaaminika kuwa mafuta ya mbono ni tiba muhimu ya nyumbani ya kupunguza makovu ya uzee.

Paka mafuta ya mbono kwenye makovu ya uzee kwenye uso na shingo kila siku asbuhi na jioni baada ya kuoga ili upate matokeo mazuri.

**Angalizo**

Endapo umeshaanza tiba ya hospitali, hakikisha usikatishe.

Lengo siyo kukufanya uache matibabu ya daktari wako. Lengo ni kukusaidia upate nafuu wakati unajiandaa kwenda hospitali.

Kama njia zote hizi hazijakupa matokeo mazuri, tafadhali nenda hospitali mapema na muone daktari.

Yawezekana kuna tatizo kubwa kiafya linalohitaji uangalizi wa karibu na vipimo zaidi.





## MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Juisi ya Karoti na Pasheni

JUISI ya karoti inayochanganywa na pasheni ni nzuri kwa afya na rahisi kutengeneza kwa muda mfupi.

**Mahitaji**

Mahitaji ya kutengeneza juisi hii ni karoti sita, pasheni tatu, mabarafu, sukari, blenda ya kusagia na chujio.

Namna ya kuandaa

Anza kuosha matunda yako na anza kumenya, karoti na ikate vipande vidogo, kata mapasheni na weka kwenye chombo kisafi na kisha mimina karoti kwenye blenda na pasheni zako na maji glasi nne kisha anza kusaga.

Saga mchanganyiko wako hadi uone zimekuwa laini kisha mimina kwenye chujio na chombo kisafi na weka sukari, ukoroge hadi ikolee.

Ukimaliza chukua juisi yako weka kwenye jagi na kisha mimina mabarafu ndani yake ma itakuwa tayari kwa ajili ya kunywa.

Unaweza kunywa juisi hii na mlo wa mchana au usiku au kitafunwa chochote.





# Tengeneza mvuto kwa aina moja ya maua

Na Restuta James

WATU wengi wanaopenda maua au bustani, wanaamini kwamba kila ua lina umuhimu wake na wangetamani wawe nalo.

Yapo maua yanayohitaji utunzaji wa hali ya juu kama jua kiasi, maji kidogo au kivuli zaidi. Yapo pia ambayo yanafaa zaidi kuweka ndani, kutokana na uwezo wake wa kusafisha hewa.

Aina hiyo ya maua inahitaji 'wakereketwa' wa maua ambao wanaweza kutenga muda mrefu kuhakikisha kila mche umestawi.

Kwa wapenda maua wasio na muda, yako ambayo yanaweza kupandwa pamoja na kutengeneza mwonekano mzuri, yakiwamo yale yanayosafisha hewa, yanayohitaji kivuli na yanayovumilia jua.

Mtaalamu wa bustani, Olipa Boaz, anasema nyumba inaweza kupandwa aina moja au mbili za maua na ikapendeza.

"Mfano, unaweza kupanda maua yasiyochanua kama vitenge, ulimi wa mama mkwe (snake plant) au jasmini inayovumilia jua na nyumba ikapendeza," anasema.

Hata hivyo, anashauri kwamba maandalizi ya bustani ya aina yoyote ya maua yanapaswa kuzingatia ubora wa udongo na mbolea, akipendekeza itumike samadi.

"Bila kujali ubora wa maua unayokusudia kuyapanda, tumia samadi badala ya mbolea ya viwandani inayoweza kuwa na kemikali. Kwa maua yanayopandwa ndani, hakikisha mbolea imeoza vizuri ili usiingize harufu mbaya ndani ya nyumba yako," anasema.



## MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# REMBESHA UZIO KUPENDEZESHA NYUMBA YAKO

UZIO ni moja ya sura ambazo zinaweza kutumika kama urembo wa nyumba kulingana na namna mhusika anavyotaka uwe kwa kutegemea na bajeti au ubunifu unaotumika kuutengeneza.

Kwa ujumla, nyumba inapozungushiwa uzio iwe ni kwa ajili ya ulinzi, usalama, faragha au muonekano, lakini unasaidia pia kuongeza thamani ya nyumba husika.

Kwa mazingira yetu ya kitanzania zipo uzio za aina mbalimbali ikiwamo za tofali, mbao, miti, makuti, chuma, aluminiam, wavu, bati na nyinginezo.

Mtaalam wa masuala ya ujenzi, Stephen Kennedy, anasema yako mambo ya kuzingatia kabla ya kuweka uzio wa nyumba yako.

Anasema ni vyema kuepuka kukurupuka kuchagua uzio kabla hujafahamu gharama za utunzaji wake na kwamba endapo utaamua kimakosa upo uwezekano wa kuharibu muonekano wa sura ya nyumba yako hata kama ni nzuri kiasi gani.

"Kwa mfano unapoweka uzio wa mbao, unatakiwa ujue kwamba unatakiwa kupakwa rangi mara kwa mara na ujue zinaoza pia baadae, kwa hiyo zinahitaji maboresho ya kila mara kwa sababu pasipo kufanya hivyo zinaharibika, hivi ni vitu ambavyo unapaswa kujua katika kila aina ya uzio unaotaka kuweka," anasema Kennedy.

Jambo lingine anasema kwamba kabla ya kutengeneza uzio wako unatakiwa ufahamu unatakiwa uwe kwa mtindo gani.


Anashauri kwamba uzio wa kurembesha zaidi katika lango kuu ikiwamo kuweka taa za rangi unasaidia kuweka muonekano mzuri wa ukuta na nyumba kwa ujumla.

Kennedy anashauri kuweka uzio wenye kuleta faragha na wa kuimarisha ulinzi katika nyumba na siyo bora uzio.

Anasema kwamba uzio unaoacha nafasi au matundu katika nyumba hauna faragha na wala hauwezi kukulinda vya kutosha, ila unakupa starehe ya kuangalia kinachoendelea nje ya makazi yako unapokuwa umejipumzisha.



# KATUNI



KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
'KAZI YA UKANDARASI WA MIGOLOFA SASA BASI! NAIONA NJIA YA KIJIJINI NYEUPEEE!
'KANJANJA'
'VILAGO'
SI UMPIGIE MKEO UMWAMBIE UMEFUNIKWA NA KIFUSI 'KALIYAKOO'
'UNIKOME'
SMOLU HAUSI
MMEO UMEMUGAJE MPAKA UME-JIACHIA?
KUZINDUA GESTI MPYA NAE ATAKUJA
HII POMBE! AU NIMEMEZA VIWEMBE?
'UKANDARASI' ULISOMEA WAPI MWENZANGU?
'HATA NAJUA BASI?'
NILIKUWA NA NDOTO YA KUJENGA GOLOFA LAKINI SASA BASI!
HAJUI HATA KUTAMKA GHOROFA ANASEMA 'GOLOFA' SIJUI KABILA GANI HUYU!
SHATI LAKO LINA VIRAKA!
KESHARAMBA 'VISUNGURA' ANAROPOKA
AACHE MZAHA TUTAMTANDIKA AKAAMKIE 'MWAISELA'
SHUA!
UNATAKA 'KURA?'
ABEE!
HIZO BARUA ZA KUWAACHISHA KAZI WATU WOTE HADI MIMI
BANGE SIO SIGARA!

# Kiongozi wa upinzani Msumbiji atoa masharti

**MAPUTO,** MSUMBIJI

KIONGOZI wa upinzani Msumbiji amesema atakubali mwito wa rais wa nchi hiyo, Filipe Nyusi, kutaka kuwepo kwa mazungumzo, kama yafanyika kwa njia ya mtandao na mchakato wa kisheria dhidi yake usitishwe.

Rais Filipe Nyusi alimualika aliyekuwa mgombea wa upinzani, Venancio Mondlane ofisini kwake kwa mazungumzo ya kuleta amani baada watu kadhaa kufariki Dunia katika maandamano ya kupinga matokeo ya uchaguzi uliofanyika Oktoba 9.

Mondlane, mgombea wa kujitegemea, alikataa matokeo hayo akisema yalichakachuliwa na kukipa ushindi chama cha Nyusi cha Frelimo.

Alisema aliondoka nchini humo kwa hofu ya kukamatwa au kushambuliwa, lakini hadi sasa hajulikani mahali aliko. Katika hotuba aliyoitoa kwenye ukurasa wa facebook, kuwa wako tayari kwa mazungumzo ya kweli na yasiyokuwa na mitego. Maofisa walimfungulia mashitaka, ikiwemo uharibifu uliosababishwa wakati wa maandamano ya wafuasi wake, ambayo yamepelekea akaunti zake za benki kufungiwa.

Sharti jingine katika waraka huo lililowekwa wazi na ofisi ya Mondlane ni kuwa mchakato huo wa kisheria lazima usitishwe.

Aidha kuna masharti mengine 20 ambayo Mondlane anataka yawepo katika ajenda ya mazungumzo, ikiwa ni pamoja na kurejesha ukweli kwenye uchaguzi na kumfungulia mashtaka yeyote aliyehusika katika wizi wa kura.

Mengine ni kuomba radhi kwa umma na fidia kwa vifo vilivyotokea wakati wa maandamano, pamoja na mageuzi ya katiba, uchumi na uchaguzi.

Hata hivyo kuna taarifa tofauti kuhusu idadi ya watu waliofariki katika maandamano hayo yaliyoambatana na ghasia.01:36 Kituo cha Demokrasia na Haki za Binadamu, ambacho ni shirika la kiraia kilisema karibu watu 65 wameuawa. Mondlane kwa upande wake alisema ni watu 60, huku Rais Nyusi, alitaja idadi ya waliofariki ni 19, wakiwemo polisi watano.

Katiba ya nchi hiyo inamtaka Rais Nyusi, kukabidhi madaraka Januari mwakani kwa mgombea wa Frelimo Daniel Chapo, ambaye tume ya uchaguzi ilisema alishinda kwa asilimia 71 zote, dhidi ya 20 ya Mondlane.

Machafuko hayo yalijadiliwa Jumatano na viongozi wa kikanda katika mkutano wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) yenye nchi 16 wanachama.

Mataifa hayo yalitoa taarifa ya pamoja kuwa inatuma salamu za rambirambi kwa serikali na watu wa Msumbiji kwa vifo vilivyotokea.

Shirika la Haki za Binadamu la Human Rights Watch liliikosoa SADC kwa kushindwa kuikemea Msumbiji kwa matumizi ya nguvu kupita kiasi.

**DW**



Jengo likiteketea katika eneo la Dnipro nchini Ukraine wakati Russia iliposhambulia kwa kombora jipya. **PICHA: ALLIANCE**

# Trump amteua Besent kuwa Waziri wa Fedha

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Marekani Donald Trump, amemteua mwekezaji Scott Bessent kuwa waziri mpya wa fedha.

Katika taarifa aliyochapisha kwenye mtandao wake wa kijamii, Trump alisema Besent ni kiongozi mwadilifu na mwenye weledi.

Besent, 62, ndiye mwanzilishi wa kundi la makampuni ya "hedge fund Key Square."

Awali alikuwa ofisa mkuu wa uwekezaji wa ofisi nyingine iitwayo "Fund Management" na anachukuliwa kuwa mtaalam wa jumla wa ulimwengu kuhusu uwekezaji.

Pamoja na kumtaka awajibike katika kupunguza deni la taifa,rais huyo mteule alisema Besent atashughulikia kukosekana kwa usawa katika biashara ya nje na kuwekea nguvu ukuaji wa uchumi.

**DW**

# Putin asisitiza matumizi kombora jipya Ukraine

**MOSCOW,** RUSSIA

RAIS wa Russia, Vladmir Putin, ameahidi kufanya majaribio zaidi ya kombora jipya la masafa ya kati lililorushwa Ukraine juzi.

Kauli hiyo ya Putin, aliitoa saa chache tu baada ya bunge la Ukraine kusitisha shughuli zake kutokana na hofu ya jengo kushambuliwa na Russia.

Siku moja baada ya Russia, kufyatua kombora jipya kwenye mji wa Ukraine wa Dnipro, Rais Putin alisema kutakuwa na majaribio zaidi ya kombora jipya la Oreshnik. Akizungumza kwenye mkutano na viongozi wa kijeshi wa nchi hiyo, alisema Russia itaanza kutengeneza makombora hayo kwa wingi.

Hata hivyo, Rais Zelensky wa Ukraine alisema tayari anatafuta mifumo mipya ya ulinzi wa angani kutoka kwa washirika wake.

**DW**

# Uganda yakiri Kenya ilihusika kukamatwa kwa Besigye

**KAMPALA,** UGANDA

UGANDA imethibitisha kwamba Kenya ilifahamu kuhusu kukamatwa kwa kiongozi wa upinzani Kizza Besigye

Msemaji wa Serikali ya Uganda, Chris Baryomunsi, alisema hakuna ukiukwaji wa sheria katika kukamatwa kwa Besigye, kutokana na serikali ya Kenya ilifahamu kila kitu.

Matamshi yake yanakuja baada ya Kenya kueleza imeanzisha uchunguzi kuhusu tukio la kukamatwa kwa kiongozi akiwa jijini Nairobi.

Uganda imelaumiwa kwa kumteka Kizza Besigye wakati akihudhuria halfa ya uzinduzi wa kitabu cha mwanasiasa wa upinzani wa Kenya.

Kizza Besigye, alisafirishwa hadi nchini Uganda na kufikishwa katika mahakama ya kijeshi Jumatano ya wiki hii.

Hata hivyo, serikali ya Kenya ilisisitiza kwamba haikuhusika na kukamatwa kwa kiongozi huyo wa upinzani.

Baryomunsi, alisema Kenya ilifahamu kuhusu kukamatwa na kusafirishwa kwa Besigye.

Aidha alisisitiza kwamba haingekuwa rahisi kumsafirisha kiongozi wa upinzani kutoka Kenya hadi nchini Uganda bila ufahamu wa serikali.

Matamshi yake yanafuatia Katibu wa Wizara ya Mambo ya Kigeni wa Kenya, Korir Sing'oei, kutaja kukamatwa kwa Besigye kama kitendo cha kujutia na kwamba uchunguzi ulikuwa umeanzishwa.

Besigye alifikishwa katika mahakama ya kijeshi jijini Kampala wiki hii na kusomewa mashtaka ya kumiliki bastola mbili pamoja na kutafuta uungwaji mkono kutoka katika mataifa ya kigeni kwa nia ya kuvuruga usalama wa Uganda.

Besigye, kanali wa zamani wa jeshi alikana mashtaka dhidi yake na kwamba yeye kama raia hastahili kushtakiwa katika mahakama ya kijeshi.

Hata hivyo, anaendelea kukaa mahabusu katika gereza la Luzira hadi Desemba 2.

**RFI**

# Wapatiwa mafunzo ufugaji kwa tija

**Na Christina Mwakangale**

WAFUGAJI takribani 20 katika kijiji cha Maguruwe, kata ya Msimbu, Kisarawe mkoani Pwani, wamepatiwa mafunzo ya ufugaji kuku wenye tija, ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, magonjwa na kujikwamua kiuchumi.

Ofisa Kilimo katika kijiji hicho, Safina Kisaka, akizungumza, jijini Dar es Salaam, alisema mafunzo yatawaongezea uelewa wafugaji hao, kwa kuwa miongoni mwa changamoto za ufugaji eneo hilo ni ukosefu wa mitaji na kushindwa kumudu bei za dawa hasa chanjo.

Pia alisema kwamba changamoto zingine ni wakazi wa eneo hilo kuzingirwa na Hifadhi ya Misitu ya Kazimzumbwi, jambo linalosababisha mifugo kuvamiwa na wanyama wakali kama vile nyoka, kutokana na ujenzi wa mabanda ya kufugia kuwa duni.

"Wafugaji wengi kwenye kijiji hiki wako mmoja mmoja, kwa hiyo mradi huu unapokwenda kuanza utarahisisha kuwa na kikundi cha wafugaji na kuwafikia kwa urahisi, ili kuwapa elimu. Huwa ninawatembelea, lakini utakuta mfugaji mmoja hadi mwingine kuna umbali mrefu kumfikia.

"Suala lingine ni tupo jirani na hifadhi, inachangia kuwapo wadudu wakali kama nyoka na mifugo kuliwa. Sasa kwa elimu hii na namna ambavyo watawezeshwa wafugaji itawasaidia kuwa na banda bora la kuku ambalo si rahisi kuvamiwa na wadudu au wanyama kutoka hifadhini," alisema Safina.

Aliongeza kwamba ufugaji kwenye eneo hilo pia unaathiriwa na mabadiliko ya tabianchi, na kusbabisha chakula cha kuku kuuzwa ghali na pia kijiji hicho kuwa kwenye mwinuko husababisha mvua zinaponyesha maji kushindwa kutumika kwenye mahitaji ya kilimo.

"Kuna wakati hata wataalamu wa kilimo tunashindwa tuwape ushauri ipi watu wetu, ardhi yetu ya mlimani na sehemu chache zina rutuba, hali ya hewa ni joto kali. Mabadiliko ya tabianchi yanasababisha kushindwa kuwaambia wapande mazao ya muda mrefu au mfupi.

"Mvua kuna wakati hunyesha kidogo, hivyo tutawambia angalau wapande mihogo, ili wasikose kabisa chakula, maana wakipanda kama mahindi mvua zisiporudi kwa wakati yatakauka, tofauti na mihogo hustahimili ukame," alisema mtaalamu huyo.

Daktari wa Mifugo kutoka kampuni ya Interchick Kitengo cha Kutumia Mbegu Bora kutoka Interchick, Dk. David Comalla, alisema kwamba kufuga kuku kwa faida pia hutegemeana na mbegu pamoja na mazingira.

"Kuzingatia ujengaji bora wa mabanda na kuzuia magonjwa na jinsi ya kupambana na mgonjwa huongeza tija na ni muhimu pia kufuata njia sahihi ya kutoa chanjo na kufuata utaratibu wa tarehe za chanjo na muda unaotakiwa kutoa chanjo kwa kuku.

"Wafugaji wanapaswa kujua mbinu ya ufugaji kisasa na kuzingatia eneo la kufugia kuku kulingana na ukubwa wa banda linalopitisha hewa na lisiloingiliwa na wadudu wakali kama vile nyoka," alisema Dk. Comalla.

Mshauri wa asasi hiyo, Dk. Elikana Kalumanga, alisema mradi huo unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kupitia miradi midogo chini ya mfuko wa Mazingira (GEF-Small Grants Programme);

Alisema malengo ya mradi huo ni kuwafikia wakazi wanaoishi jirani na hifadhi, ili wawe na shughuli mbadala wa uchumi, kupunguza utegemezi na athari kwa rasilimali za asili kama vile msitu uliopo eneo hilo wa hifadhi ya Kazimzumbwi.

"Kunapokuwa na watu wa eneo kama hilo wanaotegemea chanzo kimoja kama kilimo na ikitokea wanakwama, kutokana na mabadiliko ya tabianchi kama mafuriko, kitakachofuata ni kutegemea msitu. Ila asasi hii inakuja na shughuli mbadala wa kiuchumi na rafiki kwa mazingira bila kuwa na ujuzi mkubwa, mtaji mkubwa na shirikishi kwa makundi yote kwa vijana, wanawake na wazee, ukabuniwa mradi wa kuku.

"TaLRO pia wameungana na Interchick, ili kuwafikia wananchi hawa hata maradi ukiisha watakuwa na soko la kuuza kuku wao, baada ya kupata elimu ya ufugaji wenye tija," alisema Dk. Elikana

Happiness Temu, mmoja wa wafugaji hao, alisema anatarajia baada ya kupata mafunzo hayo pamoja na kuwezeshwa mtaji kutoka taasisi za kifedha, atafuga kwa tija, ili kuongeza kipato kwenye familia.

Pastory Msuka, mfugaji pia alisema kwamba bei ya dawa za chanjo kuuzwa kwa bei kubwa, kunawasababishia kununua dawa moja kwa kuchangishana fedha.

"Dawa moja ya chanjo ya ndui ya kuku inauzwa Sh. 12,000 utakuta hiyo fedha mimi peke yangu sina au nina kuku wachache, hitaji la dawa hiyo ni kuwa na kuku 100 nami sina, nitawatafuta wenzangu wafugaji wa kuku, ili kutimiza namba hiyo, tuchange fedha kununua dawa moja.

"Sasa ninachojiuliza hiyo dawa tunapogawana tunagawana kwa vipimo sahihi? Au ndio sababu magonjwa kwa kuku hayaishi na baadhi hufa. Ila mafunzo haya yametufungua macho," alisema Pastory.

# Wachimbaji wapewa somo kuzalisha kwa tija

**Na Maulid Mmbaga**

NAIBU Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mgeni Hassan Juma, amewataka wachimbaji wadogo kutumia Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini (GST) kupata taarifa sahihi za uwapo wa madini ili kuzalisha kwa tija.

Akizungumza juzi jijini Dar es Salaam wakati wa ufungaji wa Mkutano wa Kimataifa wa Madini na Uwekezaji 2024, alisema serikali itafanyia kazi na kuzingatia maazimio, ushauri na mapendekezo mbalimbali yaliyowasilishwa na wadau wa madini ili kuendelea kuboresha zaidi mazingira ya uwekezaji.

Mgeni ambaye alimwakilisha Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema watahakikisha wanafikia lengo la serikali la kuhakikisha madini yanaongezwa thamani nchini ili sekta hiyo iweze kuzalisha ajira nyingi na kuongeza mchango katika pato la taifa.

"Nitoe wito kwa wadau mbalimbali kuunga mokono jitihada hizo za serikali kwa kuwekeza katika shughuli za uongezaji thamani madini.

"Tanzania imebarikiwa kuwa na rasilimali ya madini muhimu, ili nchi inufaike ipasavyo na uwepo wa rasilimali hizo lazima tuhakikishe tunajenga viwanda vitakavyoongeza thamani madini hadi kufikia wazalishaji wa bidhaa kama Graphite ambayo hutumika kwa wingi kuzalisha betri kwa ajili ya magari ya umeme," alisema Mgeni.

Aliongeza kuwa ujenzi wa viwanda vya kuzalisha zao la mwisho la betri hapa nchini utaongeze ukuaji wa sekta kwa kuongeza ajira kwa watanzania na kuhamasisha teknolojia na ujuzi.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, alisema mkutano huo ulikuwa na washiriki zaidi ya 1500 na umekuwa na mafanikio makubwa ikiwemo kubadilishana uzoefu na kutangaza fursa mbalimbali za uwekezaji.

Pia alisema matarajio yao kwa siku zijazo ni kuwa na eneo maalumu la madini, huku akiwaomba wakuu wa mikoa mbalimbali kutenga maeneo makubwa kwaajili ya kujenga eneo mahususi litakalotumika kufanyia mikutano ya madini.

"Miezi kadhaa iliyopita tulizindua ripoti ya utafiti wa madini Zanzibar, na kumegunduliwa kuna madini yanayoweza kutumika kutengeneza vitu mbalimbali ikiwemo vya ndege, hivyo kupitia fursa hii naamini umma na dunia kwa ujumla itakaribishwa kuangalia namna ya kufanya uwekezaji mkubwa kwenye madini hayo," alisema Mavunde.

Naibu Waziri wa Madini, Steven Kiruswa, aliwahakikishia wawekezaji wa ndani na nje kwamba serikali itaendelea kushirikiana nao kwa shughuli mbalimbali za sekta ya madini kwa manufaa ya pande zote.

"Wizara itaendelea kuboresha taarifa za kijiolojia kuwezesha wadau kupata taarifa muhimu zitakazowawezesha kufanya utafutaji wa kina wa madini," alisema Kiruswa.

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Kila king'aacho si dhahabu, vingine chupa iliyochongwa



**Na Adam Fungamwango**

SIO kila unachokiona ni dhahabu. Ni msemo wa waswahili wakiwa na maana siyo kila unachokitazama na kuona kizuri machoni basi kipo kama kilivyo kwa ndani.

DDC Mlimani Park katika wimbo wao wa 'Nalala kwa Taabu' wana kipande kimoja kinachosema 'amini usiamini kukuchekea siyo kufurahi na we kaka...'

Maana yake anayekuchekea machoni wakati mwingine siyo kama moyo wake nao unakuchekea. Badala yake amefika husuda, chuki, roho mbaya na kisasi.

Msemo huu na wa king'aacho si dhahabu vyote vinafanana tu. Kwenye masuala ya mapenzi wapo watu wanaowaacha wapenzi wao au ndoa zao kwa ajili ya kufuata vinavyong'aa nje.

Mwanamke anaweza kushawishika na mwaume mtanashati, au mtu mwenye ushawishi kama vile maarufu, au pesa, na kumuacha mpenzi wake au mume ambaye wamekaa naye raha mustarehe.

Wengi wanadhani anavyoishi na mwenzake kwa sasa kule anakokwenda ataishi kama vile au zaidi ya vile alivyokuwa mpenzi wake.

Mwanaume naye anazuzuka na urembo na uzuri wa wanawake njiani, badala yake anajizoea mtu ambaye baadaye anakuja kujiuliza imekuje mpaka amefanya ujinga kama huo.

Wakati mwingine tayari anakuwa ameshaivuruga ndoa yake kwa kuyumba au kusambaratika kabisa. Baadaye anakuja kukuta kumbe kile ambacho ambacho alikuwa anakitarajia kutoka kwa mpenzi wake mpya sicho kile ambacho alikuwa anakipata kutoka kwa mke, mume au mpenzi wa zamani.

Tamaa na macho, mwili na mali vinakuwa vimeshampoteza, matokeo yake inakuwa kilio na kusaga meno.

Wale wanaosema siyo kila mwanaume unaweza kuwa naye na si kila mwanamke unaweza kumudu kuwa naye, kwa asilimia nyingi wako sahihi. Dunia hii Mwenyezi Mungu amempa kila mmoja wa kufanana naye.

Ukiona umeishi na mpenzi, mke au mume kwa kuanzia miaka miwili na kuendelea ujue tayari kuna muunganiko, kwani kila moja ameshajua tabia ya mwenzake na wanaendana. Kama wapenzi hawana muunganiko, yaani kufanana kwa baadhi ya tabia, hawawezi hata kuishi miezi sita ya upenzi, tayari kila mmoja ameshamkinai mwenzake.

Na hiyo ndiyo inavyokuwa kwa wale wanaowaacha mwezao kwa sababu za tamaa za kimaisha. wanapokuja kugundua kuwa kumbe walikokwenda siko wanaanza kutumia nguvu kubwa na ushawihi kutaka kurejea kule walikotoka.

Bahati nzuri aliyeachwa awe hajapata mwenza, kama amepata inakuwa balaa, mmoja anataka kurudi na aliyekuwepo anataka kung'ang'ania.

Wanamuziki wa zamani hawajaacha kulizungumzia hili. DDC Mlimani Park Orchestra katikati ya miaka ya 1980, walifyatua kibao kikali walichokiita 'Christina Bundala', utunzi wake Maximillian Bushoke.

Unazungumzia jamaa mmoja aliyeamua kumtosa mpenzi wake waliopendana na kuzoeana, Christina na kufuata warembo wa mjini kwa taama tu za kimwili.

Walimfanya walichomfanya, wakamuacha mweupe kama karatasi, akaamua kurejea kwa mpenzi wake na kumuomba msamaha.Maneno aliyokuwa anaongea wakati anaomba msamaha, ndiyo yaliyounda kibao hiki.

"Ama kweli penzi jamani, halikadiriki, hata ulipime za mzani gani. Nililichezea kamari, pendo lake Christina aaa na kujisahamu kama lingenifaa na kudumu maishani mwangu. Walinirubuni kwa maneno, nikamwacha Christina aaa na kujisahau kama angenifaa na kudumu maishani mwangu."

Hapo jamaa anaungama na kuelezea kitu kilichotokea hadi kumuacha mpenzi wake.

"Nililichezea kamari roho yangu na kuuza utu wangu, kwa wasiothamini penzi wala kujua maana ya kupendwa. Mpenzi Christina naomba unisamehe, nilinde ukiongoze kwenye penzi letu la haki. Nilihadaika na mambo ya dunia, nilihadaika na anasa za dunia, binadamu hujifunza kutokana na makosa."

Haya ni maombolezo, majuto na maombi ya msamaha kwa jamaa mpenzi wa Christina. Amejieleza vizuri sana. Hapa tatizo ni kwamba kweli alimsamehe? Christina hakuwa na mtu mwingine kwa wakati huo?

Tuwe waangalifu sana kwani si kila king'aacho ni dhahabu.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Nyuma ya Pazia-10

TAARIFA za habari kwenye televisheni, redio, mitandao ya kijamii zinaarifu kutekwa kwa mtoto wa miaka sita, Macaire, mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja Mbezi Dar es Salaam. Mashuhuda wanasema alinyakuliwa na mwanamume mmoja aliyeshiba, kujaa misuli na kukimbilia kwenye gari lililokuwa pembeni mwa barabara ya Bagamoyo, Dar es salaam, ambalo mlango wake ulikuwa wazi. Wazazi wa mtoto wanapigiwa simu na watekaji wakitaka kiasi cha Sh. Milioni 15 ili wamwachie. Jeshi la Polisi linaingia kazini kumsaka au kuwasaka watekaji. Walichogundua ni kisa cha kushangaza, kusisimua ambacho utakipata utakaposoma kila aina ya nakala ya gazeti hili, ili kuupata mkasa mzima wa tukio.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

HISIA zikaanza kuwa labda ni Mwalimu Mkuu wa Shule ya Tom Academy, Kisanga, anaweza kuwa anahusika kwa njia moja ama nyingine. Wakaamua kumuweka kando na kutomwambia chochote.

Hata hivyo bado watekaji wakawa wanapata taarifa ya vyote vinavyofanyika. Alichogundua pia ni kwamba watekaji humtumia baba wa mtoto aliyetekwa tu, Macky kutaka pesa na si mtu mwingine yoyote. Alichofanya siku ya kwanza ni kwenda Mbezi Beach kwenye shule ambayo mtoto Macaire alitekwa.

Akiwa anaendesha gari yake ndogo aina ya Volvo, XC60 alifika shuleni hapo na kuonana na mwalimu Kisanga. Alijitambulisha kama ni askari polisi wa kawaida tu ambaye anapeleleza kesi hiyo.

Alimuuliza maswali kadhaa ambayo aliona yangeweza kumfanya aanze kwa kuanzia.

Na hii ni baada ya baada ya kuambiwa kuwa alikuwa mtu wa kwanza kutoambiwa chochote kuhusu taarifa za kupeleka pesa kwa watekaji ili kuangalia kama zinaweza kusababisha kumnasa anayetoa taarifa kwao.

Kwa uzoefu wake hakuona kama mwalimu huyo anahusika kwa chochote.

Kwa sababu alikuwa na namba za baba wa mtoto aliyetekwa alimpigia ili wakutane maeneo ya Ubungo jijini Dar es Salaam.

Eddy alimpeleka moja kwa moja ofisini kwake. Ambapo alikuwa anataka kumuuliza maswali mawili matatu ambayo anadhani yangeweza kumfanya kugundua kitu.

Hata hivyo kwa Macaire hakujitambulisha kama mpelelezi, bali ni mwandishi wa habari anayefuatilia kisa hicho kwa undani kilichobeba hisia na kufutiliwa na wati wengi kwenye vyombo vya habari.

"Unaitwa nani?" Akamuuliza huku akiwa ameshika kalamu na kijitabu kidogo kwa ajili ya kuandika atakachukuwa akimuuliza "Macky Macaire."

Akajibu kwa ufupi. Licha ya kuwa alikuwa akiandika, lakini pia alikuwa amewasha kifaa chake kidogo cha kunasia sauti.

"Mtoto wako aliyetekwa anaitwa nani?" "Yeye anaitwa Macaire Macky." "Umezaa na mwanamke gani?' "Anaitwa Dora." "Unaishi naye?" "Hapana, tuliachana miaka kadhaa sasa." "Okay, kwa hiyo mkasa wote huu mnakutana polisi kila mmoja alikuwa anatoka sehemu yake?" "Ndiyo." "Kwa sasa wewe umeoa?" "Hapana, ila nina mchumba anaye nataka kumuoa hivi karibuni. Lakini kwa matatizo hata sijui kama inawezekana hivi karibuni tena." "Usiwe na hofu Macky. Mungu atasaidia tu mtoto atapatikana." "Mimi usiku na mchana naombea hivyo, lakini hapa kuna kuna kitu kinanichanganya."




**"Mtoto wako aliyetekwa anaitwa nani?" "Yeye anaitwa Macaire Macky." "Umezaa na mwanamke gani?' "Anaitwa Dora." "Unaishi naye?" "Hapana, tuliachana miaka kadhaa sasa." "Okay, kwa hiyo mkasa wote huu mnakutana polisi kila mmoja alikuwa anatoka sehemu yake?" "Ndiyo."**

"Kipi bwana Macky?" "Hawa watekaji wanajuaje kwamba pesa inayopelekwa inatoka polisi, na wanawindwa ili wakamatwe!" Akashangaa. "Unadhani bwana Macky ni kitu gani au nanianayesababisha hili. Au unayemshuku?" "Bwana mwandishi.

Mimi nadhani kuna baadhi ya askari polisi wana mtandao na hawa watu.

Wanawapenyezea siri. Wanawaambia kuwa pesa imetolewa na wapo wanaowafuatilia, ndiyo maana wamekuwa hawaji eneo la tukio ambalo wenyewe ndiyo wanakuwa wananiambia nikawawekee mzigo wao hapo." "Kuhusu Mwalimu Mkuu Kisanga huna wasiwasi naye?" Eddy akauliza.

"Mwanzoni nilipata wasiwasi huo, lakini baadaye alipotolewa kupewa habari na askari polisi lakini bado wakawa na taarifa nikajua yeye hahusiki!"

"Turudi nyuma kidogo." Eddy alimkumbusha mwanzo wa mazungumzo yao. "Mliachana mtoto akiwa na miaka mingapi?" "Miwili na nusu." Eddy hakutaka kumuuliza maswali ya moja kwa moja kuhusiana na utekaji kwani ingemfanya Macky ahisi kama mtu anayemuuliza ni zaidi ya mwandishi wa habari.

Akaamua kurudi kwenye masuala ya kifamilia. "Nani alikuwa anamlea muda wote?" "Wote wawili." "Ukiwa na maana gani?" "Ina maana tulipoachana aliondoka naye.

Lakini baadaye alikuja kunibwagia nyumbani. Akaondoka, lakini baada ya miezi kama sita hivi akaja kumchukua, tena, ikapita miezi kadhaa akaja kuniachia tena.

Yaani huyu mtoto tangu anasoma chekechea, alikuwa na sare mbili. Ya huku kwangu Kinondoni Hananasifu na yeye kwake huko Tabata, akimchukua anakwenda kusoma huko, akimrudisha anasoma huku. Suala liliisha alipoingia darasa la kwanza."

Eddy akamtazama usoni alionekana amekunja sura kama akikumbuka kitu ambacho kilikuwa kinamkera hapo zamani "Labda ulipochunguza ni kitu gani ambacho uligundua kilisababisha afanye hivyo?" Macky alionekana kutikisa kichwa hivi kwa kusikitika, ingawa kwa chati sana, halafu akatatoa tabasamu nusu ambalo halikuwa na uhalisia.

"Nilifanya hivyo kupitia mdogo wake wa kike, aliniambia alikuwa akimchukua kama akikaa nyumbani kwao akiwa hana mwanaume. Akimpata, nadhani walikuwa wanakataa kukaa na mtoto.

Kwa hiyo anakuja kunitupia huku, yeye anaenda kwa mwanaume wanaishi naye, kwa bahati mbaya alikuwa hakai nao muda mrefu, akiondoka huko ndiyo anakuja kumchukua tena huku na kukaa naye kwao. Ndiyo ilikuwa utaratibu wake.

Nadhani mtoto alipoingia la kwanza, ndugu zake wamemsema, ameacha huo mtindo, na mimi nikasisitiza kuwa mtoto nitaishi naye mimi mwenyewe." "Kwa sasa anaishi na bwana?" "Nasikia ana mchumba, amemtolea mahari na anataka kumuoa."

"Kwa hiyo wote mnaishi na hao mnaotaka kuwaona na kuolewa?" "Ndiyo mimi naishi na mwanamke ambaye nataka kumuoa, ingawa hakai mara kwa mara kutokana na kuwa ana kazi, hivyo mtoto muda mrefu anakuwa na hausigeli."

"Nitakuuliza swali la mwisho." "Uliza tu bwana mwandishi." "Mligombana nini, au mliachana vipi?" "Mimi binafsi sijui. Ila nilianza kuona vituko tu. Vituko vilianza kila siku kituko baada ya kituko, siku ya siku narudi kazini nakuta amebeba kila kitu ndani. Ilibidi nimsake, mara nikaambiwa kaenda kwa dada yake, mara wapi, kwao hakurudi. Ilibidi nianze maisha upya kwa tabu. Talaka nilimpa baadaye baada ya usuluhishi kushindikana."

Eddy aliridhika na majibu ya Macky. Akaangalia muda wake. ilikuwa imetimu saa 9:00 alasiri.

"Nikurudishe na gari yangu, au nikupe pesa za kukodi mwenyewe usafiri?" Akauliza. "Nitashukuru kama ukinipa pesa, maana hapa itakayobaki inaweza kunisaidia."

Bado hakukuwa na mwanga wowote, kwani maswali mengi aliyomuuliza yalionekana ni ya kifamilia zaidi na si ya kikazi. Yale ambayo alipaswa amuulize ili kupigisha hatua kuelekea kuwapata wahusika.

Alichopanga sasa Eddy, kesho yake ni kumapata Dora, mama mzazi wa Macaire ili naye ampe chochote ambacho kinaweza kumsaidia kwenye upelelezi wake. Ikiwezekana na yeye ajibu maswali ya kifamilia kama aliyoyajibu Macky. Alivutiwa tu kutaka kujua nani anaweza kuwa mkweli na nani muongo kuhusu kuachana kwao. Alijua kila mmoja atavutia kwake. Lakini yeye kama mpelelezi atafahamu nani anayezungumza kweli kati yao.

**Itaendelea Jumapili**

# ANDI ATUA TANZANIA KUIBUA VIPAJI

**Na Judith Julius,** Ngara

Msanii wa sanaa za maonesho kutoka Austria, Andreas 'Andi' Stecher, amewasili Tanzania kufanya kazi katika kituo cha kuendeleza sanaa cha Nafasi Art Space cha jijini Dar es Salaam.

Stecher, ambaye ni mbunifu katika kupiga ngoma, kutunga nyimbo na kuandaa muziki, atakuwa kwenye kazi hiyo pamoja na wasanii wazawa.

Msanii huyo ambaye makazi yake yako katika majiji ya Berlin nchini Ujerumani na Barcelona, Hispania atahusika na mapigo ya muziki, sauti zilizorekodiwa katika maeneo mbalimbali na kutengeneza muziki wa kuvutia.

Ushirikiano baina ya Stecher na wasanii wa Tanzania, hasa wanaofanya muziki wa Singeli, umempa hamasa ya kujihusisha na tasnia ya muziki Tanzania.





# COUNTRY WIZZY HAKUJUA ATATOKAJE

BINGWA katika muziki wa Hip Hop, Country Wizzy, amesema hakuwa na wazo la kutunga wimbo wa Wigo, lakini Whozu na S2Kizzy walichagiza kuwepo kwa ngoma hiyo.

Amesema ngoma hiyo ilitayarishwa usiku wa manane, baada ya msanii huyo kuwakuta wasanii hao wenzake wameweka muziki na sauti.

"Awali nilikuwa nawaza nitafanyaje kutunga wimbo unaohusu joto kali, lakini nilipoingia studio niliwakuta S2Kizzy na Whozu wakijaribu sauti katika midundo iliyotengenezwa. Nilirukwa akili hapohapo niliwaambia tutengeneze wimbo," amesema Country Wizzy.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### UNITED YAMTAKA PULISIC

KLABU ya Manchester United inavutiwa na winga wa AC Milan na Timu ya Taifa ya Marekani, Christian Pulisic, mwenye umri wa miaka 26, pamoja na Liverpool na West Ham.(**Kalciomercato**)

### KELLEHER ATAJWA CHELSEA

CHELSEA inapanga kumnunua kipa wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Ireland, Caoimhin Kelleher, mwenye umri wa miaka 25 katika msimu ujao wa kiangazi. (**Sun**)

### UNITED YAMBANA AMORIM

RUBEN Amorim anatazamiwa kufanya kazi kwa bajeti ndogo zaidi kuliko ya aliyekuwa kocha wa Manchester United, Erik ten Hag, na atakuwa na jukumu la kuongeza uwezo ambao haujatumiwa katika kikosi huku klabu pia ikilenga kumaliza mzunguko mbaya na wa gharama kubwa. (**Telegraph**)

### ERIKSEN KUONDOKA UNITED

KIUNGO wa kati wa Manchester United, na Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen anapanga kuondoka klabu hiyo msimu huu na hakuna mazungumzo yanayoendelea kati ya pande hizo mbili kuhusu mkataba mpya. ( **Fabrizio Romano)**

### ZIRKZEE KUMPISHA OSIMHEN

MANCHESTER United pia wanatafuta makubaliano ya kubadilishana ambayo yatamfanya mshambuliaji Mholanzi, Joshua Zirkzee, mwenye umri wa miaka 23 ajiunge na Napoli, huku straika wa Nigeria, Victor Osimhen (25), akielekea Old Trafford. (**Kalcio Napoli)**

### WEST, FULHAM VITANI

KLABU ya West Ham na Fulham zote zinavutiwa na kiungo wa kati wa Manchester City na Timu ya Taifa ya England, James McAtee, mwenye umri wa miaka 22. **(Guardian)**

### RAPHINHA ANUKIA ARSENAL

ARSENAL inavutiwa na mshambuliaji wa Brazil, Raphinha, na imeripotiwa kuandaa ofa inayokaribia pauni milioni 75. Hata hivyo, Barcelona hawako tayari kuachana na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kwa ada ya chini ya pauni milioni 83. **(Fichajes)**

### WEST HAM: KUDUS HAUZWI

LIVERPOOL na Arsenal hazitaweza kumsajili winga wa Timu ya Taifa ya Ghana, Mohammed Kudus, mwenye thamani ya pauni milioni 85 msimu ujao, kwa sababu West Ham wanapania kumbakiza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. **(Football Insider)**

### MURILLO HAENDI KOKOTE

KLABU ya Nottingham Forest itapuuza ofa zozote za kumtaka mlinzi wao raia wa Brazil, Murillo, mwenye umri wa miaka 22 katika dirisha la Januari, huku Real Madrid wakimtaja nyota huyo ni miongoni timu zinazomtaka mchezaji huyo. (**Football Insider**)


### CHIESA KUREJEA ITALIA

WINGA wa Liverpool, Federico Chiesa, mwenye umri wa miaka 27 anaweza kurejea nchini kwao Italia ifikapo Januari huku Inter Milan wakitarajia kumchukua kwa usajili wa mkopo.**(Mirror)**

### CHELSEA, CITY VITANI

CHELSEA, Manchester City na Tottenham Hotspur zipo katika mbio moja za kuwania saini ya mlinzi wa Bournemouth na Timu ya Taifa ya Ukraine, Illia Zabarnyi, mwenye umri wa miaka 22. (**Teamtalk**)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# HARRY KANE AIPIKU REKODI YA HAALAND

**MUNICH,** Ujerumani

## Ni baada ya kufikisha mabao 50 katika michezo 43 ya Bundesliga...

HARRY Kane amekuwa mchezaji kufikisha mabao 50 kwa haraka zaidi katika Ligi Kuu Ujerumani maarufu Bundesliga, akimpita aliyeweka rekodi hiyo, Erling Haaland, kwa kufunga hat tirck katika ushindi wa mabao 3-0 ambao Bayern Munich wameupata dhidi ya Augsburg hapo juzi.

Mshambuliaji huyo wa England alifunga mabao yote matatu katika kipindi cha pili, mawili kwa penalti na la tatu kwa kichwa dakika za lala salama na kufikisha magoli katika mechi 43.

Haaland alikuwa amefunga mabao 50 katika mechi 50 akiwa na Borussia Dortmund kabla ya kujiunga na Manchester City.

"Ilikuwa furaha kwa Harry Kane," alisema Kocha wa Bayern Munich, Vincent Kompany.

"Ilikuwa karibu katika kipindi cha kwanza, na kisha hutokea, nadhani mabao matatu ndani ya dakika 15. Bila shaka, anaweza kufanya hivyo.

> **"Lakini kwa mchezaji kama huyo, lazima niseme, alikuwa na nafasi nyingi ambazo angeweza kufunga zaidi."**

Kane alifunga mabao 36 katika mechi 32 za ligi msimu uliopita, ukiwa ni msimu wake wa kwanza kwa Bayern baada ya kujiunga nayo akitokea Tottenham.

Pia ulikuwa msimu wa kwanza tangu mwaka, 2012 ambapo Bayern walishindwa kutwaa taji hilo, huku Bayer Leverkusen wakiwa hawajapoteza na kunyakua taji.

Pamoja na mabao 14 ya ligi msimu huu, Kane amefunga magoli matano katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na moja katika Kombe la Ujerumani.

Bayern waliendelea kama hapo awali kwa kumiliki mpira kwa asilimia 80, lakini ilibidi wasubiri, Keven Schlotterbeck, aadhibiwe kupitia VAR kwa kumchezea vibaya, Kane.

Kane alifunga matokeo katika dakika ya tatu ya muda wa mapumziko na bado kulikuwa na wakati wa kunyakua mwingine.

Huu ni ushindi wa saba mfululizo kwa Bayern Minuch tangu Oktoba 23, mwaka huu waliposhindwa na Barcelona kwa kufungwa magoli 4-1 kwenye Ligi ya Mabingwa.

## HABARI MICHEZO



# RODRI: KUTAKIWA NA MADRID NI HESHIMA

**MANCHESTER,** England

RODRI amesema kuongezwa kwa mkataba wa Pep Guardiola ni "kichocheo muhimu" kwake kuendelea na Manchester City lakini anaacha mlango wazi kwa uhamisho wa kwenda Real Madrid kwa kuita wanaotajwa kuwa ni "heshima."

Nyota huyo ambaye aliumia misuli ya paja la kulia tangu Septemba, alisherehekea habari Guardiola amesaini mkataba wa miaka miwili kusalia kwenye uwanja wa Etihad hadi Juni mwaka, 2027.

"Ni furaha Pep ameamua kuendelea," alisema Rodri mwenye umri wa miaka 28 akiiambia redio Cadena Ser ya nchini Hispania.

"Ni wazi amekuwa kocha mwenye ushawishi mkubwa katika maisha yangu ya soka. Ni furaha kwa klabu na kwa yeye kuendelea kwa angalau miaka miwili zaidi.

"Niliposaini Manchester City mwaka 2019 waliniambia Pep angekaa kwa mwaka mmoja au miwili tu."

Alipoulizwa kuhusu mustakabali wake, Rodri, mshindi wa Ballon d'Or 2024 alisema: "Nia yangu ni kupona kwangu.

"Nimebakiza miaka miwili katika mkataba wangu, muda unakaribia wa kukaa chini na kuzungumza tena. Ni wazi kuongeza mkataba kwa Guardiola ni kichocheo muhimu ninahisi kuthaminiwa sana katika klabu kwa muda huu."

Rodri, ambaye alijiunga na City msimu wa kiangazi wa 2019 akitokea Atletico Madrid, alipoulizwa kama atafikiria kujiunga na Madrid, Rodri alisema: "Ni wazi.

"Madrid ni klabu bora na yenye mafanikio zaidi katika historia, inapokupigia simu, ni heshima. Daima unapaswa kuzingatia."

# Santo akunwa na kiwango Forest



**LONDON,** England

KOCHA wa Nottingham Forest, Nuno Espirito Santo, amesema hajashangazwa na mwanzo mzuri wa klabu yake katika msimu wa huu wa Ligi Kuu England licha ya kumaliza juu kidogo ya mstari wa kushushwa daraja msimu uliopita.

Forest, ambao walimaliza katika nafasi ya 17 kati ya timu 20 za ligi msimu uliopita, wapo nafasi ya tano katika msimamo wakiwa na pointi 19 baada ya kucheza michezo 11, watasafiri hadi London kuwafuata Arsenal walio nafasi ya nne.

Nottingham Forest hawajapoteza ugenini msimu huu, na mchezo wao dhidi ya Arsenal utatazamwa na wengi kama kipimo sahihi cha uwezo wa Nuno kwenye michezo mikubwa baada ya sare ya 1-1 dhidi ya Chelsea, mechi iliyochezwa Novemba 10, mwaka huu.

"Ninachotarajia ni wachezaji wetu kujituma kwa hali ya juu kabisa kufanya mambo sawa. Kwa nje inaweza kuwa ya kushangaza lakini kwetu? Hapana. Tunafanya nao kazi kila siku, tunajua ubora na vipaji walivyonavyo, tunataraji mengi kutoka kwao lakini tunapaswa kuwa wavimilivu na kutambua ni msimu bado mrefu na mgumu sana." alisema.

# Messi kubakia Inter Miami mpaka 2026

**FORT LAUDERDALE,** Marekani

MMILIKI mwenza wa Inter Miami, Jorge Mas, amesema anatarajia mshambuliaji, Lionel Messi, ataendelea kuwa sehemu ya timu hiyo hadi msimu wa mwaka, 2026 wa Ligi Kuu ya Soka ya Marekani.

Messi alijiunga na Inter Miami Julai, mwaka jana kwa mkataba ambao utaendelea hadi mwisho wa msimu wa mwaka, 2025.

Mkataba wa awali haujumuishi chaguo la nyongeza la klabu kurefusha hadi mwaka, 2026, na kufanya msimu ujao kuwa wa mwisho kwake.

Lakini Mas anasisitiza nyota huyo wa Argentina atasalia na timu hiyo wakati Inter Miami inapohama kutoka kwenye Uwanja wa Chase huko Fort Lauderdale hadi uwanja mpya wa Miami Freedom Park ulioko Miami.

"Messi yuko chini ya mkataba hadi mwaka, 2025, Leo na mimi tutakaa na kujadili siku zijazo," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Kama nilivyosema hapo awali, na nitarudia sasa: Natarajia kabisa katika ufunguzi wa uwanja wetu mpya mnamo 2026 na ufunguzi wa msimu wetu wa MLS wa 2026, Leo Messi atakuwa namba 10 wetu."

Messi alichukua jukumu muhimu katika mafanikio ya timu hiyo 2024, akirekodi mabao 21 na asisti 17 licha ya kucheza mechi 21 pekee za MLS msimu mzima.

Aliiongoza Inter Miami kutwaa taji la Ngao ya Mashabiki 2024 na rekodi ya ligi ya kupata pointi nyingi zaidi katika msimu mmoja.



## HABARI MICHEZO

# JKT TANZANIA FC YAREJEA DIMBANI BAADA YA SIKU 29

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE kikosi cha JKT Tanzania kinatarajia kurejea dimbani baada ya siku 29 kucheza dhidi ya Prisons katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam.

Utakuwa ni mchezo wa kwanza kwa timu hiyo, tangu Oktoba 26, mwaka huu, ilipocheza mechi ya mwisho dhidi ya Dodoma Jiji, Uwanja wa Jamhuri Dodoma, kabla ya kupata ajali Oktoba 30, mwaka huu jijini, Dar es Salaam na kusababisha majeruhi kwa wachezaji wao 11.

Baada ya hapo, Bodi ya Ligi iliahirisha baadhi ya michezo ya timu hiyo ili kuwapa muda wachezaji kuimarika afya zao.

Mechi zilizoahirishwa ni dhidi ya Simba na Namungo, lakini leo inarejea uwanjani, huku Ofisa Habari wa timu hiyo, Masau Bwire, akisema wachezaji wao wote wameshapona, wamefanya mazoezi na wapo fiti kwa mchezo huo.

"Tumejiandaa na mchezo huu, tunajua muda mrefu hatujacheza ligi, hivyo tunahitaji pointi tatu ili tujiweke vizuri katika msimamo, alisema Bwire.

JKT Tanzania ambayo imecheza michezo tisa tu, inashika nafasi ya 11 katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 10 sawa na wapinzani wao, Prisons ambao wanafuatiwa katika msimamo huo lakini wameshacheza michezo 10.

Kuelekea kwenye mchezo wa leo, Kocha Mkuu wa Prisons, Mbwana Makata, aliwapeleka wachezaji wake 'gym' kwa ajili ya kuwaongezea utimamu wa mwili kwa sababu wanakwenda kucheza na timu ya maafande kama wao.

"Lazima tuongeze dozi, wachezaji wakiwa na fiziki sawa sawa watakuwa na pumzi, spidi na kufanya kila unachowaelekeza, hasa tunapokwenda kucheza na JKT Tanzania ambayo pia ni timu ya maafande kama sisi," alisema kocha huyo.

Mbali na mechi hiyo, kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi leo Tabora United itawaalika Singida Black Stars huku Dodoma Jiji ikiwa mwenyeji wa KMC kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma.



Kiungo wa Simba, Awesu Awesu (kushoto), akiwania mpira dhidi ya kiungo mkabaji wa Pamba Jiji FC, Samuel Antwi, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza juzi. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: SIMBA**

# Twiga Stars, Ghana kundi moja

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), imepangwa Kundi C pamoja na mabingwa watetezi, Afrika Kusini (Banyana Banyana), Ghana na Mali katika Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (WAFCON).

Fainali za WAFCON zitafanyika kuanzia Julai 5 hadi 26, mwakani nchini Morocco.

Katika droo iliyofanyika jijini Rabat juzi, wenyeji Morocco wamepangwa katika Kundi A pamoja na Zambia, Senegal na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo).

Droo hiyo iliyofanyika mbele ya Rais wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Dk. Patrice Motsepe, ilishuhudiwa mabingwa mara nyingi, Nigeria wakiangukia Kundi B pamoja na Algeria, Tunisia na Botswana.

Mara ya kwanza Twiga Stars kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake ilikuwa mwaka 2010 na iliishia hatua ya makundi.

Mwenyekiti wa Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Tanzania (TWFA), Somoe Ng'itu, aliliambia gazeti hili hakuna kundi rahisi katika fainali hizo.

Alisema maandalizi kuelekea fainali hizo yameshaanza ambapo mwezi uliopita Twiga Stars ilisafiri kwenda Morocco kucheza michezo miwili ya kimataifa ya kirafiki dhidi ya wenyeji na Senegal.

"Hakuna kundi rahisi, timu zote 12 zilizofika hatua hiyo ni bora, tumejipanga kwenda katika fainali hizo kama washindani, tunaamini tutapeperusha vyema bendera ya Tanzania," alisema Somoe.

## Fadlu: Tutaimaliza...

INATOKA UK. 24

Minziro, alisema waliingia kwa kuiheshimu Simba, lakini kipindi cha pili waliamua 'kujilipua' kwa kushambulia zaidi.

"Tuliiheshimu Simba, tuliingia kwa kutengeneza mfumo wetu wenyewe kulingana na Simba ilivyo, kipindi cha kwanza hatukuwa vizuri, lakini cha pili tuliikamata mechi kwa sababu nilibadilisha mfumo na kucheza na mastraika watatu ili tushambulie zaidi, kama kutufunga mengine wacha tu watufunge, nashangaa mwamuzi kuongeza dakika mbili, kwa jinsi ilivyokuwa ilibidi ziongwezwe hata dakika 10," alisema Minziro.

Bao pekee la penalti iliyopigwa na Leonel Ateba, liliwapa ushindi Simba ambayo inaendelea kukaa kileleni na pointi 28 kibindoni, ikishuka dimbani michezo 11 huku Pamba Jiji ikisalia nafasi ya 15 na pointi nane, wamecheza mechi 12.

Ligi Kuu Bara inatarajia kuendelea tena leo kwa JKT Tanzania kuwakaribisha Tanzania Prisons wakati Tabora United itawaalika Singida Black Stars huku KMC FC itawafuata Dodoma Jiji kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma.

## Yanga yakamilisha...

INATOKA UK. 24

wanachama na mashabiki wakiungana, wakijazana uwanjani kwa kuwashangilia wachezaji wetu, tutaifanya kuwa nyapesi, wachezaji na benchi la ufundi wapo tayari kwa vita hii," alisema Kamwe.

Aliongeza wachezaji wao watarajiwa kupambana na kuhakikisha wanampokea kocha mpya kwa ushindi na si matokeo mengine.

"Wale waliokuwa katika vikosi vya timu ya taifa tunajua wengi walicheza kwa hiyo bado wana utimamu wa mwili, kuelekea kwenye mchezo dhidi ya Al Hilal, kwa maana hiyo haitampa shida sana kocha wetu, kinachotakiwa hapo ni muunganiko tu ili kupate ushindi kwenye mchezo wa kwanza ambao ni muhimu sana," alisema Kamwe.

Aliongeza hawana hofu na mchezo huo licha ya kupoteza mechi mbili mfululizo za Ligi Kuu Tanzania Bara na badala yake wataongeza umakini kuelekea mchezo huo.

"Hatuna hofu na mechi hii eti kwa sababu tulipoteza mechi zilizopita, badala yake imetufanya sasa tuwe makini kwenye michezo yote inayofuata, hatutadharau mechi wala hatutaingia uwanjani kwa mazoea," Kamwe alisema.

Klabu ya Yanga jana ilianza hamasa kwa ajili ya mchezo huo, huku Kamwe akiwataka mashabiki kujitokeza kwa wingi Jumanne ijayo kwa ajili ya mchezo huo.


"Awali tulikuwa na hamasa ya kwenda mitandao ya kijamii, lakini leo (jana), tumeanza hasama ya mtaa kwa mtaa hadi siku ya mechi," alisema.

Tayari kikosi cha Al Hilal kimewasili nchini tayari kwa mchezo huo wa Kundi A ambalo lina timu za MC Alger ya Algeria na TP Mazembe ya DR Congo.

# Michezo

Jumapili Novemba 24, 2024

Nipashe

Harry Kane aipiku rekodi ya Haaland UK. 21



Kocha mkuu wa Simba, Fadlu Davids

## Yanga yakamilisha hesabu mechi CAF

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

WAKATI Mkurugenzi mpya wa Ufundi wa Yanga, Abdihamid Moallin, akikutana na wachezaji wa timu hiyo kwa mara ya kwanza, uongozi wa vigogo hao umesema wameshamaliza 'hesabu' za kuhakikisha wanapata ushindi katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal kutoka Sudan.

Yanga itawakaribisha Al Hilal iliyoko chini ya Kocha Mkuu, Florent Ibenge, katika mechi ya kwanza ya hatua ya makundi itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Taarifa kutoka Yanga zinasema Moallin, ambaye hivi karubuni alitua Yanga akitokea KMC, alikutana na kusalimiana na wachezaji kwenye kambi ya timu hiyo iliyoko Avic Town, Kigamboni, jijini na kufanya mazungumzo na nyota wa kikosi hicho kinachotetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mkurugenzi huyo alipata nafasi pia ya kumpa mwongozo nahodha ya kikosi hicho, Bakari Mwamnyeto, ili kuhakikisha wanaenda kusaka matokeo chanya katika mechi za mashindano yote watakazocheza.

Wachezaji wa Yanga walionekana kufurahi kumwona Moallin na walimkaribisha kwa 'bashasha'.

Baadaye Moallin alisalimiana na Kocha Mkuu, Sead Ramovic pamoja na benchi lake la ufundi.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema wanafahamu mechi hiyo dhidi ya Al Hilal itakuwa ngumu na amewataka wanachama na mashabiki wao kujitokeza kuwashangilia wachezaji ili kufikia malengo.

"Ni mechi ngumu, lakini kwa ukubwa wetu na umoja wetu,



INAENDELEA UK 23

# Fadlu: Tutaimaliza Bravos

## ●●● Kocha huyo atamba Pamba Jiji FC imewapa mbinu za ushindi na...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema mechi ya Ligi Kuu iliyochezwa juzi kati ya timu yake dhidi ya Pamba Jiji na kushinda bao 1-0, Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza, imempa mwanga na mbinu za kuwaangamiza wapinzani wao, Bravos do Maquis kutoka Angola.

Simba itawaalika Bravos do Maquis katika mechi ya kwanza ya hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa Jumatano kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili, Fadlu alisema alihitaji mechi hiyo kwa malengo ya kujiimarisha kuelekea mechi hiyo ya kimataifa na kile ambacho alikitaka amekipata na sasa akili yake iko tayari kuwavaa Waangola.

"Ilikuwa lazima tucheze mchezo huu, ulikuwa muhimu mno kwa ajili ya kuweka vyema wachezaji kwa ajili mechi yetu ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Bravos do Maquis.

Aina ya mchezo ulivyochezwa, ushindani ulioonyeshwa na Pamba Jiji nilikuwa nauhitaji sana kwa sababu nilitaka wachezaji wangu wawe tayari, miili yao iwe timamu kwa ajili ya mchezo huo, na imekuwa kama nilivyojitaji. Tofauti na kama usingekuwepo kwa sababu baadhi ya wachezaji ukiacha waliokwenda kwenye vikosi vya timu za taifa, walikuwa wamepumzika bila miili yao kuwa na utayari wa mchezo," alisema Fadlu.

Kocha huyo alisema kwa sasa miili ya wachezaji wote imekaa vyema kwa ajili ya kuusubiri mchezo huo wa kwanza wa hatua ya makundi.

"Nimefarijika, nimeona wapi nitaanzia na kuishia kwenye mchezo ujao, ndiyo maana ndani ya dakika 55 za mchezo, tayari nilikuwa nimeshafanya mabadiliko mara nne, baadhi ya wachezaji nilikuwa nawahifadhi kwa ajili ya mchezo huo, wengine wameshapata utimamu kwa mwili walikotoka katika timu za taifa," Fadlu alisema.

Kuhusu mchezo huo, alisema haukuwa wa kuonyesha ufundi zaidi ya kuwaweka fiti nyota wake na kusaka pointi tatu muhimu za Ligi Kuu.

"Najivunia vijana wangu kwa kuwa tayari kupambana, tulicheza mchezo huu kwenye uwanja ambao haukuwa rafiki kwa wachezaji, uwanja ambao nyasi zilikuwa zimeliwa, matope na ulikuwa unateleza, wachezaji wangu hawakuonekana kuwa tayari kucheza kwenye hali hii ya hewa, hawakuwa na spidi, hawakuonyesha ufundi, wakati mwingine unacheza mechi kwa ajili ya kushinda, siyo mpira mzuri," alisema kocha huyo.

Aliwataka wanachama na mashabiki wa Simba kujitokeza kwa wingi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ili wajionee soka safi na ushindi pia.

"Hatutacheza hivi Jumatano, ikumbukwe tunacheza Benjamin Mkapa, tutacheza na timu ngumu lakini yenye kuonyesha ufundi, na sisi tutaonyesha ufundi," aliongeza Fadlu.

Naye Kocha Mkuu wa Pamba Jiji, Fred

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >